# Nipashe

Jumatatu Novemba 2, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580386

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**WENGI** wana magonjwa ya akili bila kujijua



UKURASA 4

**MBUNGE** mteule wa CUF afunguka

UKURASA 5

# JPM: Nina deni kwa Watanzania

**MAANDALIZI** ya kuapishwa yakamilika, viongozi kimataifa kuhudhuria, Dk. Mwinyi kuapishwa leo...*Endelea Uk. 2 & 17*



Rais mteule, Dk. John Magufuli, akionyesha cheti alichokabidhiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) muda mfupi baada ya kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Semistocles Kaijage (kushoto). Hafla hiyo ilifanyika jana, jijini Dodoma. Wengine ni Mgombea Mwenza, Samia Suluhu Hassan na Mkurugenzi wa NEC, Dk. Charles Mahera. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vyama tisa vyalilia kupatiwa ruzuku

UKURASA 3

**Polisi yatoa onyo kuandamana**

UKURASA 3

**MICHEZO** MUGALU MIEZI SITA NJE, SVEN ABADILI MFUMO UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# ...Maandalizi ya kuapishwa yakamilika

Na Augusta Njoji, DODOMA

MAANDALIZI ya kuapishwa kwa Rais mteule Dk. John Magufuli, Novemba 5, mwaka huu, yamekamilika na viongozi mbalimbali mashuhuri wa kitaifa na kimataifa wanatarajia kuhudhuria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema sherehe za kuapishwa zitafanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na maandalizi yake yamefikia asilimia 95.

"Tutaendelea kutoa taarifa juu ya viongozi wa kimataifa watakaoishiriki na mpaka sasa tumeshapokea pongezi mbalimbali kutoka nchi 20 kwa njia ya mtandao na salamu rasmi za kidiplomasia kutoka nchi nne ikiwamo China," alisema.

Aliwaomba wananchi kujitokeza kushiriki kwenye sherehe hizo na kuanza kuingia saa moja asubuhi uwanjani hapo.

"Burudani mbalimbali zitakuwapo za wasanii na za asili, tunaomba wananchi wa Dodoma wajitokeze kwa wingi," alisema.

Pia alisema Novemba 2, kutakuwa na sherehe za kuapishwa kwa Rais mteule wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, zitakazofanyika visiwani Zanzibar.

Oktoba 30, mwaka huu, Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, akitangaza matokeo ya Uchaguzi Mkuu ngazi ya Rais, alisema Rais Magufuli ameshinda kwa kupata kura 12,516,252 kati ya kura halali 14, 830,195 zilizopigwa.

Alisema katika kinyang'anyiro hicho nafasi ya pili ilishikwa na Tundu Lissu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambaye alipata kura 1,933,271.

Wagombea wengine ambao idadi ya kura zao zipo kwenye mabano ni pamoja na Leopold Mahona wa NRA (80,787), John Shibuda wa ADA-TADEA (33,086), Muttamwega Mgaywa wa SAU (14,922), Cecilia Mwanga wa Demokrasia Makini (14,556), Yeremia Maganja wa NCCR-Mageuzi (19,966), Ibrahim Lipumba wa CUF (72,885), Philipo Fumbo wa DP (8,283), Bernard Membe wa ACT-Wazalendo (81,129) na Queen Sendiga wa ADC (7,627).

Wengine ni Twalib Kandege wa UPDP (6,194), Hashim Rungwe wa CHAUMMA (32,878), Khalfan Mazrui wa UMD (3,721) na Seif Seif wa AAFP (4,635).



Mkuu wa Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kaskazini, Mkama Nangu (kushoto), akikabidhi vifaa tiba ikiwa pamoja na vitanda vya kujifungulia, mikasi ya upasuaji na vifaa vya kumpa joto mtoto mchanga baada ya kuzaliwa, vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 80 kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dk. Lucas Juma, katika hafla iliyofanyika Hospitali ya Endabash wilayani Karatu juzi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# JPM: Nina deni kwa Watanzania

Na Augusta Njoji, DODOMA

RAIS mteule Dk. John Magufuli, amesema ushindi mkubwa alioupata ni deni kubwa kwake na atahakikisha anatimiza imani ya Watanzania kwa kufanya kazi usiku na mchana.

Akizungumza jana baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Rais Magufuli, alishukuru Watanzania kwa kumwamini na kumchagua kwa kura nyingi kuwa Rais kwa awamu nyingine ambayo ni muhula wa mwisho kwake.

"Nawashukuru kwa kukipa ushindi mkubwa chama changu (CCM) katika urais, ubunge na udiwani, uwakilishi Zanzibar kwa hakika mmetuapa ushindi mkubwa sana ambao umetuachia deni kubwa sana."

Aliongeza: "Kwangu mimi nina deni kubwa kwa Watanzania, namwomba Mungu anisaidie pamoja na viongozi wenzangu katika awamu hii ya pili ya uongozi wetu, ili tutimize haja ya Watanzania waliotuamini kwa sababu kwangu mimi na wenzangu hili ni deni kubwa."

Rais Magufuli alisema: "Kupata ushindi wa asilimia 84.4 ni imani kubwa sana kwa Watanzania na nasema kwa dhati nina deni kubwa kwa Watanzania imani yao nitaitimiza kwa kufanya kazi sana usiku na mchana."

Alisema ushindi huo ni wa Watanzania wote na si wa kwake peke yake wala chama chake.

"Aliyenipigia kura na hata ambaye hajanipigia kura natumia fursa hii kuwaahidi Watanzania wote kwamba nitawatumikia bila kujali mahali wanapotoka ama tofauti zetu za dini, kabila, rangi au itikadi zetu za chama, mimi nitakuwa mtumishi wa Watanzania wote," alisema.

Aliwashukuru wagombea wote na kwamba wametekeleza haki yao ya kikatiba na demokrasia.

"Tunawashukuru kwa kutupa ushindani wa kutosha mmetusaidia kujua Watanzania wanataka nini, kukubali matokeo na kuja kushiriki hafla hii kwa kuwa ni ishara ya kukomaa kisiasa, maana siasa si vita wala ugomvi naahidi nitashirikiana nanyi kuhakikisha tunasukuma mbele gurudumu la maendeleo kwa kuwa hayana chama," alisema.

Alisema Watanzania wameipatia CCM ushindi mkubwa, kamwe haiwezi kuwa sababu ya kudharau maoni na ushauri wao.

"Tutaheshimu na kuzingatia maoni, ushauri na mapendekezo yenu hasa yetu, Tanzania kwanza, mambo mengine baadaye," alisema.

Aliwashukuru viongozi wa dini ambao waliombea taifa na likawa salama wakati wote wa uchaguzi.

"Navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha amani na usalama vinatawala kipindi cha uchaguzi na nina imani usalama utaendelea hata baada ya uchaguzi, nashukuru kwa viongozi wa nchi mbalimbali ambao baada ya matokeo wamenitumia salamu za pongezi na kututakia mafanikio mema," alisema.

Aliwapongeza Watanzania kwa kuonyesha ukomavu wa siasa na utulivu mkubwa wakati wa uchaguzi.

"Uchaguzi huu umedhihirisha ulimwengu kuwa sisi Watanzania sio tu tunapenda amani, lakini tumekomaa kidemokrasia sasa uchaguzi umekwisha kilichobaki ni kuchapa kazi," alisema.

Aliahidi kuhakikisha anatekeleza ilani kwa kufanya kazi kwa nguvu zote.

"Nashukuru vyama vingine vya siasa vilivyonipigia kura na kuacha ushabiki wa vyama vyao na wamefanya hayo kwa mapenzi makubwa kwa Watanzania, niwaombe bila kujali vyama tutangulize utanzania na kushikamana katika kujenga nchi kwa kuwa nina uhakika tunaweza na tutafaulu sana," alisema.

Alipongeza NEC chini ya Jaji Kaijage kwa usimamizi mzuri wa uchaguzi ambao umefanyika kwa ufanisi wa hali ya juu.

"Hakuna shaka kwa mtu aliyeshiriki anajua umefanyika vizuri tena kwa kiwango cha juu, vifaa vilifika kwa wakati, mwaka huu kwa mara ya kwanza kulikuwa na karatasi za kupigia kwa watu wenye ulemavu, vituo vya kupigia kura vilikuwa vingi na vya kutosha na kufanya kusiwe na misururu mirefu wakati wa kupiga kura," alisema.

Vilevile, alisema matokeo yametolewa kwa haraka hivyo kupunguza taharuki kwa wananchi na imetokana na matumizi mazuri ya TEHAMA.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, alisema siri ya ushindi wa CCM ni umoja na kuwaomba wanachama kupokea ushindi huo kama mzigo na deni kwa Watanzania.

"Watanzania tushikamane kipindi hiki kazi tuliyoifanya ni kubwa tusikubali kuchonganishwa, kutenganishwa wala kugombanishwa," alisema.

Alisema CCM wasisherehekee kwamba uchaguzi umeisha, bali watambue mwisho wa uchaguzi ni mwanzo wa uchaguzi mwingine.

Kadhalika, alisema waliochaguliwa wote wanapaswa kuwajibika na kuzingatia nidhamu ya chama na kuwatumikia Watanzania.

## HABARI KITAIFA

# Vyama vyalilia kupatiwa ruzuku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VYAMA visivyo na uwakilishi bungeni vimemwangukia Rais Mteule, Dk. John Magufuli, kuviwezesha ruzuku ili kusaidia shughuli za kiutendaji ndani ya chama.

Akizungumza kwa niaba ya wagombea 10 wa urais ambao walishiriki uchaguzi mkuu mwaka huu, kwenye hafla ya kukabidhiwa cheti cha ushindi Rais Magufuli, mgombea wa ADC, Queen Sendiga, alisema vyama hivyo vinaomba uwezeshaji ruzuku japo kwa asilimia kidogo, ili kusaidia kufanya shughuli za kiutendaji ndani ya chama.

"Tunaomba utufikirie na kama inawezekana ili tupate chochote ili kufikia malengo ya kuwafikia Watanzania kipindi hiki," alisema.

Aidha, alimpongeza Rais Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kishindo na kwamba vyama hivyo vimeridhika na mchakato wa uchaguzi na kuahidi kumuunga mkono.

"Sisi tunaahidi kukupa ushirikiano wa hali na mali na pale utakapoona inafaa tuijenge Tanzania kwa pamoja kwa kuwa Watanzania wanahitaji maendeleo na maisha mazuri na haya yanapatikana kwa kutunza amani ya nchi iliyopo,"alisema.

Aliwaasa Watanzania kutambua kuwa uchaguzi umeisha, hivyo wajikite katika kujenga nchi.

Naye, mgombea wa NRA, Leopold Mahona, alitumia nafasi hiyo kuwashukuru Watanzania kwa kufanya uchaguzi kwa amani na kufanya maamuzi.

"Nampongeza Magufuli kwa ushindi wa kishindo namwombea aendelee kuchapa kazi, na muunga mkono kwamba nipo tayari kufanya naye kazi," alisema.

Awali, akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles Mahera, alisema katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kata nne kati ya 3,956 hazikufanya uchaguzi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wagombea wa kata tatu kufariki na kata moja ilikumbwa na tatizo la karatasi za kupigia kura.

Alisema mfumo unaotumika kwa uendeshaji wa uchaguzi ni mgombea anayepata kura nyingi ndio anatangazwa kuwa mshindi kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na Sheria ya Uchaguzi.

"Pia mfumo mwingine utatumika uwiano wa kura ambapo hutumika kupata wabunge na madiwani wa viti maalum,"alisema.

Alibainisha kuwa kwenye uchaguzi huo kulikuwa na waangalizi wa uchaguzi na asasi za kiraia, ambapo Tume ilitoa vibali 97 kwa asasi za ndani ya nchi na taasisi 20 za kimataifa zilizokidhi vigezo.

# Polisi yaonya maandamano

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini limeonya kuhusu maandamano yanayodaiwa kupangwa kufanyika kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu wa Jumatano.

Mkoani Pwani, limewaonyawafuasi wa vyama vya siasa kuacha kuhamasisha maandamano, ambayo hayana kibali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Wankyo Nyigesa, ndiye aliyetoa onyo hilo, wakati akizungumzia kauli za baadhi ya viongozi wakuu wa vyama vya siasa vya upinzani siku moja baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kukamilisha kutangaza matokeo ya uchaguzi uliofanyika Oktoba 28.

Wankyo alisema viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani ambao hawakuridhika na matokeo kufuata sheria na si kuhamasisha maandamano.

Alisema yeyote atakayeingia barabarani kuandamana hatua za kisheria zitachukuliwa kwa maelezo kuwa maandamano hayo yakifanyika yatachangia uvunjifu wa amani.

**SHINYANGA**

Mkoani Shinyanga, limewaonya viongozi wa vyama vya siasa pamoja na wafuasi wao, wasijaribu kufanya maandamano ya kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, badala yake waende mahakamani kupinga matokeo hayo.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alitoa onyo hilo jana kutokana na matamko yanayotolewa na viongozi wa kisiasa kutaka kufanya maandamano nchi nzima yasiyo na kikomo kuanzia leo ya kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu.

Alisema maandamano hayo ni batili na kwamba viongozi hao walipaswa kufuata sheria ya kupinga matokeo hayo mahakamani badala ya kufanya maandamano ambayo yana viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga halitasita kamwe kuchukua hatua kali za kisheria, kwa kikundi chochote kile cha kisiasa chenye nia ya kuvuruga amani ya nchi," alisema Magiligimba.

"Kama wagombea hawajaridhika na matokeo ya uchaguzi mkuu wafuate sheria, kanuni na taratibu za nchi na kupeleka malalamiko yao mahakamani na siyo kufanya maandamano ya bila kikomo yenye viashiria ya uvunjifu wa amani," aliongeza.

Pia, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kutojiingiza kwenye maandamano hayo, bali waendelee na shughuli zao za kila siku za kujiingizia kipato na wasiwe na hofu ikiwa ulinzi utaimarishwa kila kona.

**MWANZA**

Mkoani Mwanza Jeshi hilo limewataka wananchi kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii, licha ya kuwapo taarifa za baadhi ya vyama vya upinzani kutangaza kufanya maandamano nchi nzima.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Muliro Jumanne Muliro, akizungumzia na waandishi wa habari, alisema kazi ya uchaguzi imeisha na sasa wananchi waendelee na shughuli zao.

Alisema jeshi hilo limejiandaa kuimarisha ulinzi kukabiliana na wanaotaka kuleta vurugu kwa namna yoyote.

Muliro alisema, mtu yeyote atakayethubutu kuandamana atakabiliana na polisi bila kujali cheo chake.

Kamanda Muliro alisema, wananchi wema hawatakiwi kupata hofu yoyote badala yake waendelee na kazi zao.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi halitamvumilia mtu ama kikundi cha watu kinachotaka kuleta fujo mkoani kwake, kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria za nchi.

Viongozi wa juu wa vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi mkuu vikitangaza kufanya maandamano yasiyokuwa na kikomo kwa nchi nzima.

Viongozi hao waliohamasisha na kutangaza maandamano wanatoka vyama vya ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

**RC TANGA**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, amepiga marufuku maandamano ya vyama vya siasa mkoani kwake, akisema kitendo hicho kinaweza kusababisha uvunjifu wa amani.

"Tunachohitaji ni amani, uchaguzi umeisha na kilichobaki ni kuangalia shughuli nyingine za maendeleo zinavyokwenda, sasa tuwe watulivu," alisisitiza Shigela.

Shigela alisema hataki kuona mikusanyiko yoyote mkoani humo, kwa sababu tayari uchaguzi umemalizika na walioshinda wameshatangazwa, huku akiwataka walioshindwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kukubali matokeo.

**Imeandikwa na Marco Maduhu, Shinyanga, Julieth Mkireri, Pwani, Richard Makore Mwanza na Luli George, Tanga.**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO

TANGAZO LA KUITWA SHAURINI

SHAURI LA MADAI NAMBA:...104..2020

Mdai: MONICA RICHARD

DHIDI YA

Mdaiwa: GODFREY BROWN

Kwa: GODFREY BROWN

Ombi la Mdai: MONICA RICHARD

Madai ya: Taraka,Mgawanyo wa Mali, Usimamizi wa watoto na Matunzo ya watoto nne 300,000/= kwa mwezi

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 15 mwezi 11 mwaka 2020 saa 08:00 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 30 mwezi 10 mwaka 2020.

HAKIMU



MEDICAL TEAMS International

**Procurement Opportunities**

Tender for Framework Agreements

Medical Teams International is Non-Government Organization (NGO) which was founded in 1979, providing life-saving medical care for people in crisis, such as survivors of natural disasters and refugees.

Medical Teams International, Kasulu Tanzania is inviting interested suppliers to express their interest to supply MTI with items per description below. All interested parties are invited to participate.

| | |
|---|---|
| **Procuring Entity:** | Medical Teams International |
| **Tender No:** | MTI20/GEN PROC/001 |
| **Tender Name** | Invitation to Tender for Framework Agreements |
| **Reference Number** | **CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS** |
| PP/MTI-TAN/01/2020 | Supply of general stationery. |
| PP/MTI-TAN/02/2020 | Supply of office supplies. |
| PP/MTI-TAN/03/2020 | Supply and maintenance of photocopiers, scanners, computers, printers, Uninterruptible Power Supply (UPS), laptops, software, toners and other ICT accessories. |
| PP/MTI-TAN/04/2020 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PP/MTI-TAN/05/2020 | Supply, installation and maintenance of fire and security alarms equipment and security systems. |
| PP/MTI-TAN/06/2020 | Supply of Fuel (Diesel & Petrol) |
| PP/MTI-TAN/07/2020 | Supply of bottled water, dispensing machines and maintenance. |
| PP/MTI-TAN/08/2020 | Supply of motor vehicle/cycle parts and accessories. |
| PP/MTI-TAN/09/2020 | Supply of airtime and scratch cards. |
| PP/MTI-TAN/010/2020 | Supply of office furniture's and fixtures. |
| PP/MTI-TAN/011/2020 | Medicines |
| PP/MTI-TAN/012/2020 | Medical Consumables |
| PP/MTI-TAN/013/2020 | Medical Equipments |
| **Reference Number** | **CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES** |
| PP/MTI-TAN/014/2020 | Provision of catering services. |
| PP/MTI-TAN/015/2020 | Provision of air travel, reservations and ticketing services. |
| PP/MTI-TAN/016/2020 | Provision of sanitary, fumigation, pest control and cleaning services. |
| PP/MTI-TAN/017/2020 | Provision of internet services. |
| PP/MTI-TAN/018/2020 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PP/MTI-TAN/019/2020 | Provision of security services (guards, dog patrols and security survey). |
| PP/MTI-TAN/020/2020 | Servicing, repair and maintenance of vehicles and motorcycles |
| PP/MTI-TAN/021/2020 | Vehicle Hire-minibus, pickups, hardtop Landcruiser's |
| PP/MTI-TAN/022/2020 | Provision of printing services |
| **Source of Fund** | Bureau of Population, Refugees and Migration & UNHCR |
| **Eligible Firms** | National (Registered in Tanzania) |
| **Method of Procurement** | National Competitive Bidding |
| **Mode Application** | Via Email; procurementtz@medicalteams.org (Please send an introduction email for document inquiry) |
| **Deadline** | 11th November 2020 4:30PM |
| **Bids Submission** | Effective 12rd October to 11th November 2020 |

*"Daring to love like Jesus, we boldly break barriers to health and restore wholeness in a hurting world"*

215940502

# Wengi waugua magonjwa ya akili bila kujitambua

**Na Mwandishi Wetu**

MTAALAMU wa magonjwa ya akili, amesema watu wengi wanaugua ugonjwa wa akili, lakini hawajui na hata wanapohisi dalili hawaendi hospitalini kutibiwa.

Miongoni mwa mambo yanayochangia magonjwa hayo ni ugumu wa maisha, kukata tamaa, wasiwasi na hisia mbaya dhidi ya wengine.

Dk. Isaak Lema wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUHAS), ametaja moja ya tatizo la afya ya akili ambalo linawakumba wengi ni sonona.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akitoa mafunzo maalumu kwa watu wanaougua magonjwa yasiyoambukiza (NCD).

"Ukiwa na sonona dalili zinazoweza kujitokeza ni kukosa hamu ya kula, tendo la ndoa, hali ya kutotaka kujumuika na wengine, kuwa na mawazo ya kutaka kujiua, kuhisi uchovu, kukosa usingizi na kushindwa kutekeleza majukumu ya kawaida ya kila siku," alisema.

Dk. Lema alitaja dalili nyingine kuwa ni huzuni endelevu, kusahau matendo ya muda mfupi, kushindwa kufanya uamuzi, kukosa umakini, kujihisi kuwa na hatia kwa mambo yasiyokuhusu na maumivu ya mwili yasiyoweza kubainika kwa vipimo hospitalini.

Dk. Lema alisema watu wengi hujikuta na matatizo hayo, lakini hawaendi hospitalini kutibiwa na matokeo yake huathirika zaidi kiafya na kuwasababishia hasira, ukichaa na hata kujaribu kujiua.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasioambukiza (TANCDA), Prof. Andrew Swai, alisema moja ya njia za kuepuka sonona ni kuzungumza na watu wa karibu juu ya matatizo yanayokukabili.

Alisema wakati mwingine sonona inasababishwa na mambo ya kuletwa na watu wengine, hivyo akashauri kukabili hali hiyo kwa kuwadharau kwa sababu mwishowe watachoka na wala maneno yao hayawezi kudhuru mwili.

"Kumbuka ule wimbo unaosema 'Waache waseme, mwisho watachoka," alionya Prof. Swai.

Hatua nyingi alisema ni mtu kukubali matatizo ya dunia na kuyakabili kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuomba ushauri.

Alionya kuhusu kuwa na tamaa ya mambo ambayo yapo nje ya kipato na hasa kwa kutaka kuwa na mali kwa vile mwenzako anayo.

Alionya kuwa sonona ni miongoni mwa magonjwa yanayowasumbua wengi na yanaweza kuwa chanzo au kuhatarisha zaidi hali ya kiafya kwa wanaougua NCD.

Alitaja miongoni mwa NCD kuwa ni kisukari, shinikizo la damu, saratani, siko seli, pumu na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa.

Washiriki wa mafunzo hayo wengi walielezea kukabiliwa na sonona mara kwa mara, hivyo kuiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwatuma wataalamu wa afya ya akili kwenye kliniki zao, ili waelimishwe na kupatiwa tiba.

"Tukiwapata wataalamu hawa itatusaidia tusiathirike zaidi na magonjwa haya," alisema Mwalimu Getruda Mgindo, ambaye anaugua shinikizo la damu pamoja na figo kwa zaidi ya miaka 20.



Watalii 531 kutoka Urusi wakishuka katika ndege ya Shirika la Azur juzi, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**


www.imbank.co.tz
invest@imbank.co.tz

"Bank's Tariff
(Applicable from 03rd Sept, 2020)
ALL CHARGES ARE TAX EXCLUSIVE EXCEPT TISS CHARGES

I&M Bank LIMITED
YOU'LL LOVE THE DIFFERENCE

| | Local Currency (LCY) | Foreign Currency (FCY) |
|---|---|---|
| **Monthly Ledger Fees / Maintenance Fees** | | |
| Current Account, Bonanza Account | TZS 15,000 | TZS 15,000 Equivalent |
| Dunduliza Savings Account, Salary Account, Young Savers Account | Free | Free |
| Msomi Student Account | Free | Free |
| I&M Express Account | Free | Free |
| Noble Current Account | TZS 20,000 | US$, EUR, GBP 10 |
| Kwetu Current Account | TZS 20,000 | US$, EUR, GBP 10 |
| Kwetu Savings Account | Free | Free |
| Tunaweza Womens - Savings Account, Current Account, Group Account | Free | Free |
| **Minimum Initial Deposit Required for Account Opening** | | |
| Current Account, Bonanza Account | TZS 100,000 | US$, EUR, GBP 100 |
| Dunduliza Savings Account, Young Savers Account | TZS 20,000 | US$, EUR, GBP 20 |
| Salary Account | Free | Free |
| Msomi Student Account | TZS 10,000 | N/A |
| I&M Express Account | TZS 10,000 | N/A |
| Noble Current Account | TZS 100,000 | US$, EUR, GBP 100 |
| Kwetu Current Account | Nil | Nil |
| Kwetu Savings Account | Nil | Nil |
| Tunaweza Womens - Savings Account | TZS 10,000 | US$, EUR, GBP 20 |
| Tunaweza Womens - Current Account, Group Account | TZS 30,000 | US$, EUR, GBP 50 |
| **Transaction Fees - per entry** | | |
| Current Accounts | TZS 400 Per transaction | TZS 400 Equivalent Per transaction |
| Dunduliza Savings Account, Salary Account, Young Savers Account | Free | Free |
| Salary handling/Bulky internal transfers charges | TZS 500/ Per salary | TZS 500 Equivalent/ Per Salary |
| Msomi Student Account | Free | Free |
| I&M Express Account | Free | Free |
| Kwetu Current Account | Free (iCLick internet banking charges apply) | Free (iCLick internet banking charges apply) |
| Kwetu Savings Account | Free (iCLick internet banking charges apply) | Free (iCLick internet banking charges apply) |
| Noble Current Account | Free | Free |
| Tunaweza Womens - Savings Account, Current Account, Group Account | Free | Free |
| Salary handling/Bulky internal transfers charges (Noble account and Tunaweza Account) | Free | Free |
| **Statement Charges** | | |
| Current account and Overdraft Account (Monthly statement) | Free | Free |
| Savings Account (Quarterly Statement) | Free | Free |
| E-statement (Infomail) | Free | Free |
| Interim Statement - current year | TZS 1,200 / page | FCY 1 / page |
| Interim Statement - previous year | TZS 1,200 / page | FCY 1 / page |
| **Cash Deposit** | | |
| Small Denomination TZS 500 1,000 2,000 | Below TZS 30M: Free Above TZS 30M charge 1% | |
| US$ Cash deposits - Current Account and Overdraft Account | | Free |
| US$ Cash deposits - Dunduliza Savings Account | | Free |
| Deposit Denomination less than 50 EUR/US$ | | 4% |
| Deposit Denomination less than 20 GBP | | 4% |
| Tunaweza Womens - Savings Account | Below TZS 20M: Free; Above TZS 20M charge 1%. | Free |
| Tunaweza Womens - Current Account, Group Account | Below TZS 30M: Free; Above TZS 30M charge 1%. | Free |
| **Cash Withdrawals** | | |
| Cash withdrawals at counter (Current and Overdraft Account). Daily Limits | Upto TZS 5M: Free; Above TZS 5M: charge 0.12% Max TZS 100,000/- | Upto US$ 10,000/- 0.5% above 1% |
| Cash withdrawals at counter (Dunduliza Savings Account). Daily Limits | Upto TZS 1M: TZS 2,000/-; TZS 1M - TZS 5M: charge TZS 3,000/-Above TZS 5M: charge 0.12% Max TZS 100,000/- | Upto US$ 5,000/- per day is Free, above that 1% |
| Noble Current Account Cash withdrawals at counter | Free Upto TZS 50M. Above that 0.05% | Upto US$ 10,000/- per day is Free. Above that 0.5% |
| Tunaweza Womens - Savings Account (Cash withdrawals at counter restricted to 1 per month. ATM and iCLick transactions are not restricted) | Upto TZS 10M: Free; Above TZS 10M: charge 0.12% Max TZS 100,000/-US$; | Upto US$ 5,000/- per day is Free, above that 1% |
| Tunaweza Womens - Current Account, Group Account | Upto TZS 10M: Free; Above TZS 10M: charge 0.12% Max TZS 100,000/-US$: | Upto US$ 5,000/- per day is Free, above that 1% |
| **Funds Transfers** | | |
| Internal Funds Transfers (Non Mobile Banking) | Free | Free |
| **Inward Remittances** | | |
| Incoming Funds Transfers (TISS) | Free | Free |
| Incoming Funds Transfers (TT) | Free | Free |
| Income EFT Local | Free | Free |

| | | |
|---|---|---|
| **Outward Remittances** | | |
| Outgoing Funds Transfers (TISS/EAPS) | TZS 10,000 | US$ 10 |
| Outward EFT - External (Single/bulk) | TZS 3,000 | N/A |
| Outgoing Funds Transfers (TT) | 0.1% min equivalent to US$ 40/- & Max US$ 100 | 0.1% min FCY 40/- & Max FCY 100/- |
| Brisk Transfer | | US$ 20 |
| Outgoing funds Transfers Rapidex - Existing Customers (Routed Through Account) | | US$ 6 |
| Outgoing funds Transfers Rapidex - Walk-in Clients | | US$ 8 |
| **Cheque Services** | | |
| 25 Leaves | TZS 18,000 | TZS 18,000 Equivalent |
| 50 Leaves | TZS 36,000 | TZS 36,000 Equivalent |
| 100 Leaves | TZS 72,000 | TZS 72,000 Equivalent |
| Counter cheque | TZS 10,000 | TZS 10,000 Equivalent |
| Stop Payment - per instruction (Single Continuous cheque series) | TZS 50,000 | TZS 50,000 Equivalent |
| Revoke Stop Payment Instruction | TZS 10,000 | TZS 10,000 Equivalent |
| Note: Cheque book destruction charges apply if any requested cheque book remain uncollected by customer within 6 months | | |
| **Account Closure Charges** | | |
| Current accounts | TZS 35,000 | TZS 35,000 Equivalent |
| Dunduliza Savings Accounts | TZS 10,000 | TZS 10,000 Equivalent |
| **Cards Related Charges (Visa Debit Cards)** | | |
| Annual charges | TZS 6,000 | TZS 6,000 Equivalent in FCY |
| Card replacement | TZS 15,000 | TZS 15,000 Equivalent in FCY |
| New pin request (Pin regeneration) | TZS 2,000 | TZS 2,000 Equivalent in FCY |
| Cards uncollected and destroyed (after 3months) | TZS 15,000 | TZS 15,000 Equivalent in FCY |
| Cash withdrawal-I&M ATM per withdrawal | TZS 700 | TZS 700 Equivalent in FCY |
| Other bank ATM withdrawal -In Tanzania | TZS 1,500 | TZS 1,500 Equivalent in FCY |
| Other bank ATM withdrawal - Outside Tanzania | TZS 5,000 | TZS 5,000 Equivalent in FCY |
| Annual Safe Deposit Lockers at Oysterbay branch (Only in TZS) (Size in CMs - Height x Width x Depth) | | |
| **Annual Safe Deposit Lockers at Oysterbay branch (Only in TZS) (Size in CMs - Height x Width x Depth)** | | |
| Small Size (41.5 x 13 x 10) | TZS 150,000 | |
| Medium size (41.5 x 16.5 x 13) | TZS 200,000 | |
| Large size (41.5 x 33.5 x 12) | TZS 300,000 | |
| Extra Large (41.5 x 33.5 x 27) | TZS 400,000 | |
| **Annual Safe Deposit Lockers at Nyerere Branch (Only in TZS) (Size in CMs - Height x Width x Depth)** | | |
| Locker Type D (18.9 x 26.3 x 49.2) | TZS 300,000 | |
| Locker Type 2D (18.9 x 53 x 49.2) | TZS 600,000 | |
| Locker Type 4D (40.4 x 53 x 49.2) | TZS 1,000,000 | |
| Locker Type B (15.9 x 21 x 49.2) | TZS 200,000 | |
| Locker Type 2B (15.9 x 42.3 x 49.2) | TZS 500,000 | |
| Locker Type 4B (32.1 x 42.3 x 49.2) | TZS 800,000 | |
| Locker Type 2B1 (32.1 x 21 x 49.2) | TZS 500,000 | |
| **Appraisal Fees For Credit Facilities** | | |
| **Overdraft (P/A)** | | |
| Limits below TZS 100M | 1% | |
| Limits from TZS 100M - TZS 500M | 1% | |
| Limits from TZS 500M - TZS 1,000 | 1% | |
| Limits from TZS 1,000M and above | 1% | |
| TL above 5years | 1% | |
| Temporary over draft per quarter | 1% Flat | |
| Minimum Appraisal fees | NIL | |
| Advances against Deposits | NIL | |
| **Term Loan (Flat)** | | |
| Limits below TZS 100M | 1% | |
| Limits from TZS 100M-TZS 500M | 1% | |
| Limits from TZS 500M-TZS 1,000 | 1% | |
| Limits from TZS 1,000M and above | 1% | |

| Fixed Deposit - TZS | 3 Month | 6 Month | 12 Month |
|---|---|---|---|
| 1,000,000 - 4,999,999 | 3.0% | 3.5% | 4.5% |
| 5,000,000 - 99,999,999 | 3.5% | 4.5% | 5.5% |
| 100,000,000 - 499,999,999 | 4.5% | 5.5% | 6.5% |
| 500,000,000 and above | 5.0% | 6.0% | 7.0% |
| **Prime Lending Rate** | | | |
| TZS 19% | USD 10% | | |

# Mbunge mteule asema CUF haijamzuia kuingia bungeni

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE mteule pekee wa Chama cha Wananchi (CUF), Shamsia Mtamba (pichani), Jimbo la Mtwara Vijijini, amesema chama chake hakijatoa msimamo wowote wa kumzuia kuingia bungeni.

Mtamba alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu.

"Mimi na chama changu hatuna kauli wala tamko lolote la kukataa kuingia bungeni, ninachofahamu nimechaguliwa na



wananchi wangu na kinachofuata ni kwenda kuwawakilisha kama walivyoniamini," alisema Mtamba.

"Kama kuna baadhi ya vyama wanasema hawataenda bungeni, mimi chama changu hakijatoa kauli yoyote."

Alisema siri kubwa ya yeye kuchaguliwa katika nafasi hiyo ni kuongea vizuri na wapigakura pamoja na namna alivyoelezea sera za chama chake kwa wananchi hao.

Alisema atajitahidi kupaza sauti yake kadri anavyoweza ili isikike kwa kutetea Watanzania.

"Nitajitahidi kupaza sauti yangu kadri ninavyoweza na ninaamini kwamba itasikika. Nilikuwa mbunge wa viti maalum kupitia chama hiki cha CUF, lakini mwaka huu nikaona niingie kwenye jimbo na nashukuru nimepata," alisema Mtamba.

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, ni Mtamba (CUF) na Aida Kenani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliofanikiwa kushinda kati ya viti 264 vya majimbo yote nchi nzima.

Chama Cha Mapinduzi (CCM), ndicho kilichofanikiwa kushinda majimbo 262.

Akihojiwa na chombo kimoja cha habari, mbunge huyo mteule alisema, "Sijajisikia vizuri sana kuwa mpinzani peke yangu maana najua kuna mambo hayatakwenda vizuri. Nitajitahidi kupaza sauti yangu kuwasemea wananchi."

# NCCR-Mageuzi kutoa msimamo matokeo ya uchaguzi mkuu

**Mwandishi Wetu,** MOSHI

CHAMA cha NCCR-Mageuzi, kimesema kinafanya tathmini kuhusu uchaguzi mkuu tangu ulivyoanza hadi kutangazwa kwa matokeo, kabla ya kutoa msimamo wake kuhusu matokeo yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wiki iliyopita.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya chama hicho, Anthony Komu (pichani), alisema:

"Tumepata malalamiko mengi nchi nzima kutoka kwa wanachama wetu kuhusiana na mchakato mzima wa uchaguzi wa mwaka huu kuanzia kipindi cha kampeni, uchaguzi ulivyofanyika mpaka wakati wa kutangazwa kwa matokeo," alisema.

"Tunafanya uchunguzi kuhusu uchaguzi ulivyoendeshwa, maana tuna malalamiko mpaka ya maandishi; makamishna wa Tume huko juu walionyesha kila dalili ya kuwa uchaguzi utakuwa ni wa huru na haki ila katika utekelezaji wake."

Alisema kuna kasoro nyingi zilizojitokeza na kwamba wanaodai kushinda wana wajibu kukaa na wale wanaodaiwa kushindwa ili kudumisha umoja walio na Watanzania.

Komu ambaye alikuwa ni mgombea wa ubunge Jimbo la Moshi Vijijini, alisema pamoja na mgombea urais wa chama hicho, Yeremia Maganja, kukubali matokeo na kuweka saini kuthibitisha hilo, hiyo haizuii NCCR-Mageuzi kutoa taarifa yenye msimamo wake kuhusiana na uchaguzi



mkuu huo.

"Suala la Maganja kukubali matokeo na kutia saini, hakuhalalishi wala kuharamisha matokeo, wala uamuzi wake huko haubatilishi madai ya haki ya kitaifa ikiwamo ile ya kutaka Tume huru ya uchaguzi," alisema.

Akijibu swali kuhusu chama hicho kuyakubali au kuyakataa matokeo yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na kama watashiriki maandamano ya kupinga matokeo hayo, Komu alisema kuwa kwa nafasi yake, hana mamlaka ya kutoa msimamo wa chama.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WATER**
**RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION AGENCY (RUWASA)**
**LOSAA-KIA WATER SUPPLY TRUST**
**P. O. Box 171, HAI, Phone: (+255) 737036952**
**Email: jstambuli2000@gmail.com**

## VACANCY FOR WATER TRUST MANAGER AND TRUST ASSISTANT TECHNICAL SUPERVISOR

Losaa-KIA Water Supply Trust (LKWST) under RUWASA is a full autonomous Water Utility based in Hai District, responsible for the provision of basic demand of adequate clean and safe drinking water and improvement of hygienic situation. LKWST is looking for dynamic, results driven individuals to fill in the position of ***"Manager" and "Assistant Technical Supervisor".***

**1.0: Position: Manager (1 Post)**
**1.1: Purpose of the Job:**
This is a Managerial position in which the position holder will be responsible with the entire managerial aspects of water supply, community hygienic proportion and sound environmental affairs as well as Human Resources management.

**1.2: Main duties and Responsibility**

i. The Chief Executive of Trust responsible for administrative issues on day to day basis,
ii. Responsible to prepare annual budgets and recommend staffing levels required for the Trust and submits them to the Board for approval,
iii. Regularly review actual performance against approval plans and budgets and submit reports to the Board detailing performance with recommendations for actions necessary to correct adverse variance,
iv. Responsible to ensure all Trust's financial transactions are authorized and controlled in accordance with the agreed procedures and that proper system of internal control is maintained,
v. Responsible for preparing and submits to the external Auditor the annual accounts of the Trust within four months after the end of the financial year,
vi. Responsible to ensure existence of organization structure, manning levels, recruitment and selection procedure and staffing of the Trust with the right number of staff who are properly qualified and experienced
vii. Responsible for ensuring water supply and good hygienic practice according to Trust's agreed performance and public health standards,
viii. Evaluated currently and future water demand of Trust's commanding areas and recommend to the Board planned options of meeting the expected demands,
ix. Responsible for maintaining and repairing, planning and construction of both extension and new water projects with friendly environmental considerations,
x. Recommending new or amendment of policies, regulations and by-laws to the Board of Trust for:
   - Fixing water tariffs and revenue collections,
   - The control of water quality by developing procedures for water quality monitoring and ensure co-coordination sampling of raw water and chlorinated water supplies to ensure compliance with the prescribed standards of drinking water,
   - The operations and maintenance of all water sources (Springs/rivers) and water treatment (chlorination) works and water network,
   - Operations and maintenance of all Vehicles, machines, plants and equipment used in running water supply networks,
   - Control and properly manage all assent of Trust as per public property management guides
xi. Trough RUWASA District Manager, links the Trust with other Government and Non Government Institutions taking into considerations that possible soundest public relations with all stakeholders such as customers, suppliers are well observed and maintained,
xii. Liaison with Water Basin Offices to ensure efficient and effectiveness in management of water sources within Trust's water catchment areas
xiii. To perform any other duties as may be assigned by the Board and Government Official as per Trust's constitution and Memorandum of Understand.

**1.3: Minimum Job Requirements**
**1.3.1: Qualification**
- First degree in Engineering in any of the following fields; Water Resources, Civil, Environmental or any Water Related Discipline ,
- Should be registered with Professional Engineering Board as Professional Engineer as well as having more than Five years of relevant working experience, of which three years must be in management position,
- Should have a background in water supply utility or related engineering aspects as well as have analytical, broad minded, creative and unquestionable integrity,

**1.3.2: Key competence**
- Proven computer knowledge and skills,
- Demonstrated good leadership qualities,
- Ability to work in team work and under pressure
- High level of initiative, creativity and integrity

**1.4: Age Limit**
The applicant should be below 50 years when lodging this application

**1.5: Nature of Employment**
Five years (5) renewable depending on the performance

**1.6: Remuneration**
This position attracts competitive salary plus other fringe benefits

**2.0: Assistant Technical Supervisor (1 Post)**
**2.1: Purpose of the Job**
This is a supervision position in which the position holder will be responsible to supervise the entire allocated area of water supply networks and community hygienic proportion.

**2.2: Main duties and Responsibility**
Assist the Technical Supervisor in performing his Duties
Performs other related duties as he/she may be assigned by his/her superiors

**2.3: Minimum Job Requirements**
**2.3.1: Qualification**
- Holder of full Technician Certificate in Civil Engineering (FTC) or Diploma in Water Supply and Sanitation Engineering or Diploma in Irrigation Engineering.
- Working knowledge of proper water works plumbing methods and techniques.
- Computer literate.

**2.3.2: Key competence**
- Good in computer knowledge and skills,
- Able to communicate effectively both in English and Swahili languages.
- Proactive, good communicator, team player and self-motivated.
- Able to work under minimum supervision

**2.4: Age Limit**
The applicant should be below 35 years when lodging this application

**2.5: Nature of Employment**
Five years (5) renewable depending on the performance

**2.6: Remuneration**
This position attracts competitive salary

**3.0: Mode of Application**
A written application along with Curriculum Vitae to include reliable contacts (emails and day time working telephone), applicant's recent passport size and copies of all relevant certificates, transcripts and testimonies, names and addresses of at least three (3) reputable referees to reach the undersigned by 30th November, 2020 before 16:00 hours.

**Manager,**
**Losaa-KIA Water Supply Trust (LKWST)**
**P.O.Box 171,**
**Hai – Kilimanjaro.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi acheni kupepesa macho sheria 17 viwanjani

**LIGI** Kuu Bara imeingia raundi ya tisa kwa mechi nne kupigwa jana, Kagera Sugar ikiikaribisha Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, wakati Ruvu Shooting ikiwa mwenyeji wa Coastal Union kwenye dimba la Mabatini mkoani Pwani.

Ni Simba na Yanga pekee ndizo zimecheza mechi nane baada ya mchezo wao wa watani wa jadi kuahirishwa awali kutokana na kupisha Kalenda ya Fifa mwezi uliopita, wakati huu Azam FC ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa. Azam yenye pointi 22 sawa na Yanga, tofauti yake ya mabao ya kufunga na kufungwa ni 11 dhidi ya tisa ya 'Wanajangwani' hao waliopo nafasi ya pili, lakini wakiwa mchezo mmoja nyuma ya vinara hao.

Wakati ligi msimu huu inaanza hadi kufikia raundi ya tano, malalamiko kwa waamuzi yalionekana kupungua tofauti na msimu uliopita, jambo ambalo wadau na mashabiki wa soka walianza kurejesha imani kwa kujitokeza kwa wingi kuhudhuria viwanjani baada ya msimu uliopita mahudhurio kudorora.

Hata hivyo, wakati huu timu zikijiandaa kuelekea raundi ya 10, tayari tumeshuhudia Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ikiwafungia baadhi ya waamuzi na kutoa adhabu kwa baadhi ya wachezaji kwa kushindwa kutekeleza sheria 17 za soka wakiwa katika majukumu yao uwanjani. Kwa ujumla tunaipongeza TPLB kwa kuchukua hatua hiyo mapema jambo ambalo litaendelea kujenga imani kwa mashabiki na wadau wa soka ambao walianza kurejesha hamasa kwa timu zao kwa kuhudhuria kwa wingi viwanjani kuzisapoti tofauti na msimu uliopita ambao wengi walisusa moja ya sababu ikiwa ni kutofurahishwa na maamuzi ya waamuzi.


Tunatambua Ligi Kuu Bara msimu huu imekuwa ngumu kutokana na kila timu kupania kupata matokeo mazuri mapema katika mzunguko huu wa kwanza, ili kujiweka katika mazingira mazuri ama ya kutwaa ubingwa au kujinusuru na janga la kushuka daraja. Na kama ilivyo desturi kwa baadhi ya waamuzi wa soka nchini, ponapojitokeza ushindani kama huo hutumia mwanya huo kuzifinyanga kwa makusudi sheria 17 za soka wakiwa na lengo la kuzibeba baadhi ya timu ama kwa mapenzi yao au kurubuniwa fedha ili kufanya hivyo. Hivyo, tunawataka waamuzi kutokupepesa macho katika kutenda haki na umakini wawapo uwanjani kwa kufuata sheria 17 si tu ili kuhamasisha mashabiki kuendelea kuhudhuria viwanjani kwa wingi, bali pia kuliwezesha taifa kupata bingwa halali atakayekwenda kuiwakilisha vema nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Lakini tunawakumbusha waamuzi kumulika macho matumizi makubwa ya nguvu yanayotumiwa na baadhi ya wachezaji uwanjani ambayo husababisha wachezaji wa timu pinzani kupata majeraha na kushindwa kuzitumikia timu zao.

Ikumbukwe mashabiki na wapenzi wa soka wanapohudhuria viwanjani, hufuata burudani na kutaka kuona mpira ukichezwa na si rafu zisizo za msingi zinazotokana na matumizi makubwa ya nguvu, yanayochangiwa na waamuzi kufumbia macho baadhi ya matukio yanayostahili kutolewa kwa adhabu ya kadi ama ya njano au nyekundu. Tunaamini waamuzi wakiongeza umakini kwa kutofumbia macho baadhi ya matukio uwanjani ambayo yanastahili kutolewa adhabu, wachezaji watatekeleza vema majukumu yao uwanjani kwa kufuata sheria 17 za soka na mashabiki kufurahia burudani na kuzidi kuhamasika kwenda viwanjani hivyo klabu kunufaika kwa kupata mapato makubwa.

Tunatambua kuna baadhi ya makosa ya kibinadamu na hayo hayana budi kuvumiliwa na TPLB, klabu pamoja na mashabiki, lakini Nipashe tunatamani kuona dakika 90 zinapomalizika katika kila mechi, kila timu na wapenzi wa soka wakitoka uwanjani bila malalamiko kwa waamuzi. Aidha, waamuzi hawana budi kutambua kuwa mashabiki kwa sasa wana ufahamu mkubwa wa sheria 17 za soka kutokana na kufuatilia mechi za kimataifa katika luninga, hivyo ni wakati kwao kubadilika kwa kuchezesha kwa haki ili kutowapoteza tena viwanjani, lakini kuliwezesha taifa kupata wawakilishi bora wa michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kwa Morrison wamefanikiwa, waamuzi lindeni wachezaji

**NILIKUWA** nasikiliza adhabu za Bodi ya Ligi nchini (TPLB) kwa wachezaji waliofanya makosa mbalimbali kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Pamoja na mambo mengine, mchezaji Salum Kimenya amefungiwa mechi tatu na faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kumpiga ngumi mchezaji wa Simba, Bernard Morrison.

Mwingine ni mchezaji Shaaban Msala, ambaye naye amepewa adhabu kama hiyo kwa kosa la kumpiga teke Morrison. Mchezaji mwingine aliyepewa adhabu kama hiyo ni Juma Nyosso ambaye yeye kosa lake lilikuwa ni kumkanyaga Morrison mguuni kwa makusudi.

Halafu Morrison wenyewe naye amepewa adhabu kama hiyo kwa kosa la kumpiga ngumi Juma Nyosso. Ukiviangalia vitendo hivi vilivyofanyika, unaweza kuviona vya kawaida. Siyo kama havipo kwenye soka, lakini ukiangalia kwa jicho la tatu kuna maswali kadhaa ya kujiuliza.

Watu wa intelijensia wakikutana na vitu kama hivi, basi wao wanakuwa wamepata kazi ya kufanyia uchunguzi. Vitendo vyote hivi ukiviangalia japo ni matukio tofauti, lakini vinahusiana na mchezaji mmoja tu, Morrison.

Kimenya kampiga ngumu Morrison. Msala kampiga teke Morrison. Nyosso kamkanyaga Morrison. Na mwishoni sasa Morrison mwenyewe kampiga ngumi Nyosso. Hapa kuna tatizo.

Ni kwamba Morrison amekuwa ni hatari sana kiasi cha baadhi ya wachezaji wa timu pinzani wameamua kumkabili kwa kumpiga ngumi na mateke? Je, ni kwa sababu ya uwezo mkubwa wa kisoka na ubunifu pamoja na chenga za maudhi alizonazo?

Kama ni hivyo, mbona kuna wachezaji kama Clatous Chama, Luis Miquissone wa Simba na Haruna Niyonzima wa Yanga wana uwezo kama wa Morrison kwani wao hawawindwi na ngumi na mateke? Haya ndiyo mambo ambayo watu wa intelijensia wangejiuliza.

Nadhani wangekuja na majibu kuwa Morrison amekuwa akiwindwa kwa sababu gani. Hapo ndipo ingebidi kufanya uchunguzi zaidi.

Inavyoonekana ni kwamba, huenda Morrison asingempiga Nyosso ngumi adhabu hizi zisingetolewa. Nakumbuka hata kwenye mechi ya Simba dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, mchezaji mmoja wa maafande hao alimkanyaga Morrison kwa makusudi mkononi.

Ilikuwa baada ya kukwatuliwa na mchezaji mmoja. Baada ya kuanguka chini, mwingine alikuja na kumkanyanga kwa makusudi mkononi. Ilikuwa bado kidogo amvunje. Cha ajabu vitendo hivi vikaendelea bila kuchukuliwa hatua, lakini baada ya Morrison kuonekana kama vile amechoka kuonewa, ingawa hii nayo si sawa alichokifanya, ndipo adhabu zikaanza kutolewa.

Inawezekana kabisa lengo lilikuwa ni kumfungia Morrison. Lakini kila matukio ya nyuma yakiangaliwa yanaonekana kuwa yeye mwenyewe ameshafanyiwa mambo kama hayo mara kadhaa.

Pamoja na hayo yote, naipongeza TPLB kwa kutoa adhabu hizo zote ili iwe fundisho kwa wachezaji wengine ambao wanataka kuufanya mchezo wa soka uonekane kama mchezo wa kihuni. Naipongeza Bodi ya Ligi pia kwa kuwafungia waamuzi, hususan Shomari Lawi, ambaye amekuwa na tabia ya kuvurunda kwenye mechi zake mbalimbali. Hata hivyo, si Lawi tu, waamuzi wengi wa Tanzania wamekuwa na tabia ya kuogopa kuchukua hatua stahiki pale baadhi ya wachezaji wanapoufanya mchezo wa soka kuwa kama mchezo wa 'rugby' ambao una matumizi makubwa mno ya nguvu.

Unaweza kuona mchezaji akamkanyaga mwenzake au kumchezea rafu mbaya, lakini mwamuzi eti anakwenda kusuluhisha na si kutoa kadi japo ya njano. Kuna wakati waamuzi wanaochezesha mechi wanazifanya ziwe ngumu wenyewe na baadaye zinawashinda.

Mchezaji anayecheza rafu mbaya, hawapewi hata kadi, upande wa pili wanaamua na wao kurudisha, mwamuzi sasa anashindwa afanye nini kwa sababu awali aliachia upande mmoja, hivyo anakuwa na kazi ya kuamua vurugu zaidi kuliko kuchezesha soka.

Kama waamuzi wa Kibongo wangekuwa wanatoa kadi za njano mapema kwa rafu za kipuuzi, wachezaji wangeogopa na kucheza soka kwa kufuata sheria 17 za soka. Ukiangalia waamuzi wa Ulaya huwa hawalei mchezaji. Waamuzi wa huko wao hawapigi filimbi kwenye matumizi ya nguvu za mwili kwa mwili tu. Lakini wako makini sana kwenye rafu za mguu wa mchezaji mmoja kumgusa mwingine wakati akiwa na mpira au hana mpira.

Hata rafu moja mbaya tu, inaweza kukupeleka nje na si lazima ianze ya njano. Hii ni tofauti na waamuzi wa Tanzania ambao rafu anaweza akaacha, na matumizi ya nguvu ya mwili kwa mwili akapiga filimbi.

Ni wajibu sasa kwa waamuzi wa Tanzania kuwalinda wachezaji kwa kuangalia pia afya zao na si kuchezesha tu. Mpira ndiyo kazi za wachezaji hao zinazowafanya waishi na familia zao, hivyo kuacha watu kufanya fujo, ngumi, mateke na rafu za kuvunjana ni kutoutendea haki mpira wa miguu.

## HABARI KITAIFA



Gari la maliasili na utalii likiwa linachukua mwili wa Rodgers Willson ambaye aliuawa na tembo. **PICHA: ASIRAJI MVUNGI**

# Tembo wavamia kijiji, waua mwalimu

**Asraji Mvungi,** MWANGA

KUNDI la tembo ambalo idadi yake haijajulikana, limevamia makazi ya watu katika Kijiji cha Kwako kilichoko Tarafa ya Jipendea wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro na kuua mtu mmoja na kusababisha taharuki kubwa kwa wananchi.

Nipashe ilifika eneo la tukio na kushuhudia tukio hilo na kuzungumza na baadhi ya wananchi wakiwamo waliokuwa na mwenzao aliyeuawa waliyemtaja kwa jina la Rodgers Willson, ambaye ni mkazi wa mkoa wa Mbeya.

Wanakijiji walisema kijana huyo ni mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kwangu iliyoko kwenye kijiji hicho, na kwamba alikutana na tembo hao alipokuwa anarejea nyumbani kwake majira ya kati ya saa mbili na saa tatu usiku.

Mmoja wa wananchi hao, Nassoro Lucas, alisema waliachana na mwalimu huyo majira ya saa mbili usiku na alimuaga kuwa anakwenda nyumbani, lakini anapitia kibandani kuchukua mahitaji yake.

"Mwalimu tulikuwa tunaangalia mpira pamoja na baadaye tuliagana vizuri, nasikitika kuambiwa kuwa ameuawa na tembo," alisema Nassoro.

Diwani Mteule wa Kata ya Kwakoa, Kiende Athumani Mvungi, alisema wananchi wa eneo la karibu na yalikotokea mauaji hayo walisema walisikia kelele zinazoashiria kuwapo kwa tembo hao, lakini hawakuweza kuchukua hatua zozote kwani limekuwa ni jambo la kawaida kwa wanyama hao kuvamia maeneo yao.

Alisema hata hivyo, asubuhi alilazimika kuendelea kufuatilia na ndipo akapewa taarifa kuwa kuna mtu amekutwa ameuawa katika eneo hilo na walipofika wakamkuta ni mwalimu huyo.

Alisema walikuta mwili wake una majeraha mengi ya kuburuzwa na kukanyagwa na tembo hao na pia pembeni walikuta viatu vyake, chakula aina ya chipsi na soda ya pepsi.

Mtendaji wa kata hiyo, Dadi Khamisi, alisema tatizo la tembo katika eneo hilo limekuwa la muda mrefu na walishatoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika na hatua za kuwakabili zimeshachukuliwa, lakini tatizo bado ni kubwa.

"Kikosi cha watendaji wanaohusika na wanyamapori walikuja hapa na kujaribu kukabiliana na tembo hawa, lakini inavyoonekana wanazidiwa nguvu kwani kwa sasa mbinu wanazotumia wameshazizoea na hawaogopi tena hata baruti ama mavuvuzela yanayotumika kuwafukuza tembo hao, na kwamba jitihada za ziada zinahitajika.

Mkuu wa Shule ya Kwangu, Augustino Manento, alisema mwalimu huyo ambaye ni wa kujitolea, alikuwa anafundisha somo la Hisabati katika shule hiyo kwa mwaka mmoja sasa na ni miongoni mwa walimu waliotegemewa sana katika shule hiyo.

Aidha, mwalimu Manento alisema licha ya tembo hao kuzurura kwenye maeneo ya shule wakati wa usiku, pia wakati mwingine wamekuwa wakifika shuleni hapo mchana na wamekuwa wakilazimika kuwazuia wanafunzi kurudi majumbani kwao kama hatua ya kuwaepusha na tembo hao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwakoa, Abdala Hasani, ameziomba idara zinazohusika kufanya operesheni ya kuwarudisha tembo hao kwenye maeneo yao kwani kwa sasa wanasababisha wananchi kujifungia ndani na kushindwa kufanya shughuli zao za kila siku.

Baadhi ya wanawake wamesema wanakabiliwa na hatari kubwa zaidi kwani uwezo wao kukimbia wanapokutana na makundi hayo ni mdogo, na wameziomba idara zinazohusika kutatua tatizo hilo kwani hali ni mbaya, na kwamba wako tayari kuhamia maeneo mengine kama wakiwezeshwa ili kuepukana na majanga hayo.

Kwa mujibu wa viongozi wa kijiji hicho, tembo hao ambao kila mwaka wamekuwa wakiingia katika eneo hilo nyakati za kiangazi na kisha kurejea katika maeneo yao katika kipindi hiki cha miaka miwili, wamedumu katika eneo hilo na zipo taarifa kuwa wameshakuwa na watoto.

Akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Wanyamapori nchini, Dk. Maurusi Msuha, alisema hatua za kuwakabili tembo hao zinaendelea na watahakikisha kuwa wanaondoka katika eneo hilo.

Kwa sasa wananchi wa eneo hilo wanalazimika kujifungia majumbani mwao kuanzia saa 12 jioni na kutokana na tembo hao kuzagaa katika maeneo mengi, na baadhi yao wamesema wamekuwa wakiwafuata hata majumbani mwao.

Kwa mujibu wa viongozi wa eneo hilo, katika kipindi cha mwaka huu watu watatu wameshauawa na wengine zaidi ya watano wamenusurika na wamepata ulemavu ukiwamo wa kuvunjwa miguu na maeneo mbalimbali ya miili yao.


NICOL
The Economic Shield of the Nation

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 6 WA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)**

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 6 wa mwaka wa Wanahisa wa National Investments Plc (Nicol) utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 21 Novemba, 2020 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (JNICC), uliopo mtaa wa Shaban Robert, Dar es Salaam, Tanzania kuanzia saa 4:00 asubuhi. Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:**

6.1. MATANGAZO NA AKIDI
6.2. KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
6.3. KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 5 ULIOFANYIKA TAREHE 26 OCTOBA 2019.
6.4. YATOKANAYO NA MKUTANO WA 5 WA WANAHISA
6.5. KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2019.
6.6. TAMKO LA GAWIO LA NUSU MWAKA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA 2020.
6.7. KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI.
6.8. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2020
6.9. KUPOKEA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MABORESHO KATIKA DAFTARI LA ORODHA YA HISA.
6.10. MENGINEYO.

**MAELEZO MUHIMU:**
Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano ni lazima wawasilishe nyaraka zifuatazo: nakala ya stakabadhi yake ya Hisa (Depository Receipt) pamoja na Kitambulisho cha Kitaifa au kitambulisho cha mpiga kura au pasipoti.

Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofi¬si za NICOL zilizopo Mikocheni B, 11 Serengeti Road (kwa njia ya mkono au barua pepe **invest@nicol.co.tz**) kabla ya saa 4 asubuhi Ijumaa ya tarehe 20 Novemba 2020.

Fomu ya uwakilishi (Proxy forms) itakua inapatikana katika ofisi za NICOL au unaweza kuzipakua katika tovuti ya NICOL's (**www.nicol.co.tz**).

**Kwa idhini ya Bodi**

Arphaxad GA Masambu
CEO/ Katibu wa Kampuni

National Investments PLC
11 Serengeti Road, Mikocheni "B"
P.O. Box 7465 Dar Es Salaam
Phone: +255 22 2701436/2701348, 0682 720 679
E-mail: invest@nicoltz.com

# Salome Makamba aachiwa kwa dhamana

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limemwachia kwa dhamana aliyekuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia (CHADEMA), Salome Makamba.

Aidha, linawashikilia watu wengine tisa, kwa tuhuma za kutaka kuchoma moto nyumba ya Mbunge Mteule wa jimbo hilo (CCM), Patrobasi Katambi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alitoa taarifa hiyo jana, kuwa Makamba alijisalimisha polisi jana, / juzi majira ya saa mbili usiku, baada ya kusikia kwenye vyombo vya habari akitafutwa na jeshi hilo.

Alisema baada ya kujisalimisha alidhaminiwa, huku jeshi hilo likiendelea kuwa shikilia watu tisa, ambao wanadaiwa kuwa ni wafuasi wa Makamba, waliokwenda nyumbani kwa Katambi kutaka kumchoma moto. "Oktoba 30 majira ya saa 7 usiku tuliwakamata watu wanne, kwa tuhuma za kutaka kumchoma moto Mbunge Mteule wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, na sasa tumeongeza wengine watano na kufika tisa," alisema Magiligimba.

Alisema jeshi hilo, linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo, na upelelezi ukikamilika watu hao, akiwamo Makamba watafikishwa mahakamani.

Oktoba 30, mwaka huu Katambi, akiwa amelala nyumbani kwao eneo la Ushirika, ilidaiwa alinusurika kifo, baada ya vijana wawili kutaka kuichoma moto nyumba hiyo, na kuishia kukichoma moto choo cha nje na kisha kukimbia baada ya kukurupushwa.




Baadhi ya watoto wakiokota mabaki ya vyakula kwenye sehemu ya kuhifadhi taka eneo la Uhindini jijini Dodoma, jana, kuachwa kwa taka hizo bila kuondolewa mapema na mamlaka zinazohusika inahatarisha makundi hayo, kwa sababu kuna wengine wanatupa taka zenye sumu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkuu wa KKKT ataka nchi zingine ziombewe corona

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewataka Watanzania kuziombea nchi nyingine zinazokabiliwa na ugonjwa wa homa kali ya mafua (Covid 19), kama walivyofanya kwa Tanzania.

"Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusikia maombi yetu, lakini Tanzania pekee kuwa salama haitoshi, sisi ni sehemu ya dunia, hivyo nawasihi tuungane pamoja kuendelea kuwaombea wenzetu wanaokabiliwa na gonjwa hili, hasa majirani zetu, ili nasi tuwe salama zaidi," alisisitiza.

Askofu Dk. Shoo aliyasema hayo wakati akigawa dawa na vifaa tiba kwa hospitali na vituo vya afya vya kanisa hilo juzi jijini Arusha.

Dawa na vifaa tiba hivyo vilitolewa na wafadhili mbalimbali, likiwamo Shirika la Misaada la Norway (NORAD), vikiwa na thamani ya Sh. milioni 300, vimegawanywa kwa hospitali 24 na vituo vya afya 6 vinavyomilikiwa na kanisa hilo nchini.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa vifaa hivyo na dawa, Mkurugenzi wa Huduma za Afya katika kanisa hilo, Dk. Paul Mmbando, alisema vifaa hivyo vimetolewa na marafiki wa kanisa hilo, ikiwa ni sehemu ya kusaidia athari zilizosababishwa na mlipuko wa corona mapema mwaka huu.

Aliwashukuru marafiki hao kwa msaada huo, akisema hospitali nyingi za kanisa hilo zililazimika kuingia madeni, ili kukabiliana na mlipuko huo na athari zake.

"Kutokana na mlipuko wa corona, vifaa tiba na dawa vilipanda bei ghafla kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji, huku mapato ya hospitali nyingi yakapungua sana, hivyo msaada huu umekuja wakati mwafaka," alisema Dk. Mmbando.

Dk. Mmbando alitoa wito kwa marafiki wengine na wasamaria wema kuendelea kuzisaidia hospitali na vituo vya afya ambavyo vinalazimika kuwasaidia watoto yatima, wajane na wananchi wengine wenye mahitaji maalum ambao wanahitaji huduma za afya.

Vifaa tiba na dawa vilivyogawanywa ni vifaa tiba kwa ajili ya madaktari na wahudumu wa afya (PPE) pamoja na mavazi maalum ya kufanyia upasuaji, mabuti ya maabara, dawa za kutuliza maumivu na dawa kwa ajili ya kuongeza kinga ya mwili.

Kanisa hilo linamiliki mtandao mkubwa wa utoaji wa huduma za afya nchini likiwa na hospitali 24 ikiwamo ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyopo Moshi na vituo vya afya na zahanati 148.

## Viongozi wa dini watoa neno kwa vyama vya siasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa madhehebu ya dini Mkoa wa Dodoma wamewataka viongozi wakuu wa vyama vya siasa walioshindwa na kugomea matokeo ya uchaguzi mkuu wa urais, waende kwenye vyombo vya sheria na siyo kutaka kuandamana na kutoa kauli za uchochezi zinazoashiria uvunjifu wa amani.

Aidha, viongozi hao wa dini wameviomba pia vyombo vya dola kuhakikisha vinadhibiti wanasiasa na wafuasi ambao wanaochochea vurugu na kuharibu amani ya nchi kwa kutaka kuandamana kutokana na kutoridhishwa na matokeo ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Kauli hizo zilitolewa na viongozi hao walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Philadelphia Gospel Assembly Tanzania na nchi za Ulaya na Bara la Afrika, Dk. Yohana Masinga, alisema viongozi wa vyama wa siasa ambao hawajaridhishwa wanatakiwa kutafuta haki yao kwa kutumia vyombo vya sheria.

Alisema haki yoyote inapatikana kwa kutumia njia za kisheria ikiwamo mahakama na siyo kwa kuvuruga amani na utulivu uliopo.

Naye Shekhe wa Mkoa wa Dodoma Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mustaph Rajabu, alisema kuwa haki yoyote inapatikana kwa kutumia vyombo vya mahakama, na siyo kwa kususia na kuleta chokochoko inayoashiria uvunjivu wa amani na kuhamasisha maandamano ya mitaani.

Shekhe huyo alisema vyombo vya kisheria vipo na vimeweka ili kutafuta haki, hivyo malalamiko yao wanapaswa kupeleka huko.

Aidha, kwa upande wa Watanzania kujiepusha na kauli hizo ambazo zilizotolewa na viongozi hao kwa kuwa zinaweza kuwahatarisha maisha yao.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Pentekost Maombezi Tanzania, Living Mwambapa, alisema kuandamana siyo dawa, kinachotakiwa kudai madai yao kwa kupitia vyombo vya kisheria.

Askofu mstaafu wa Kanisa la EAGT Ipagala, Evance Chande, alisema kuwa Watanzania wanachohitaji kuwapata viongozi waliowachagua kwa maslahi ya maendeleo, hivyo kwa wale walioshindwa wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa walioshinda ili kuijenga nchi.

HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza wanafunzi wa udaktari kupewa ushirikiano

**Na Julieth Mkireri**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Nyamhanga, kutoa maelekezo kwa waganga wakuu wa mikoa, ili wanafunzi wa taaluma ya udaktari wanaoenda kupata mafunzo kwa vitendo wapewe ushirikiano na kusimamiwa inavyotakiwa.

Jafo alitoa agizo hilo, juzi, wakati akiweka jiwe la msingi katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi City tawi la Chanika, jijini Dar es Salaam.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea maelezo ya vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wa Chuo cha City wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo kutoka kwa uongozi wa chuo hicho.

Waziri Jafo alimtaka Nyamhanga kuhakikisha anatoa maelekezo hayo mapema, ili wanafunzi wanaenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali na vituo vya afya.

"Hawa wanafunzi wanatakiwa kupewa ushirikiano kwenye maeneo wanayoenda, ili hata wanapopata ajira wawe wamekamilika kwa nadharia na vitendo," alisema.

Aidha, alisema, atafanyia kazi suala gharama wanazotozwa wanafunzi wanapoenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali na vituo vya afya.

"Nitafuatilia kuanzia sasa zisipofutwa basi zisiwe mzigo ili kila mwanafunzi amudu kulipia na kupata mafunzo kwa vitendo kwa wakati katika hili pia maelekezo yatafika kwenye hospitali," alisema. Mkuu wa chuo hicho, Fei Diwani, alisema tawi hili lilianzishwa Septemba mwaka huu, ikiwa ni moja ya mikakati ya chuo hicho kuongeza udahili wa wanafunzi na kuwapa fursa Watanzania wengi.

Alitaja vikwazo wanavyokabiliana navyo ni baadhi ya vituo vya afya kutowaruhusu watumishi wake kufundisha wanafunzi wawapo katika vituo vyao wakati wa mafunzo kwa vitendo licha ya kuwa na mkataba na kufanya malipo.




Watoto wakipata maelezo Benki ya NMB tawi la Oyster Plaza jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya kufunga mwezi wa huduma kwa wateja. Mtoto huyu pamoja na wengine 25 walipewa elimu ya fedha na benki hiyo, iliyolenga kuwajengea utamaduni endelevu wa kuweka akiba tangu wakiwa watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati ya amani yavishukia vyama kuandamana

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KAMATI ya Amani Mkoa chini ya Sheikh wa Mkoa wa Geita, Alhaji Yusuf Kabaju, imekemea matamko ya baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ya kuitisha maandamano na badala yake wafuate taratibu zilizopo, ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani.

Alhaji Kabaju amewaasa wanaodhani hawakutendewa haki kufuata taratibu zilizopo badala ya kuandamana na pia kuwaasa vijana kutokubali kutumiwa na kama wanaona ni vema wao viongozi wa kisiasa ndio watangulie na familia zao kuandamana.

Wadau wa amani wakiwamo viongozi wa dini kutoka madhehebu tofauti yanayounda kamati hiyo, wanasema kukemea hatua hiyo inalenga kutoa fursa kwa viongozi waliochaguliwa kisheria na kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuanza kuwatumikia wapiga kura wao, ili kutekeleza ahadi walizokuwa wanazitoa wakati wa kampeni.

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, NEC kupitia wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo na kata iliwatangaza wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Geita kilishinda ubunge majimbo yote saba na udiwani kata zote 122 za mkoa wa Geita.

## Watoto wapewa elimu kuweka akiba, nidhamu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO wamepatiwa elimu ya utamaduni chanya wa kuweka akiba na nidhamu ya fedha.

Watoto hao wamepata elimu hiyo, walipokutanishwa na Benki ya NMB wakati wa kuhitimisha mwezi wa huduma kwa wateja.

Akizungumza wakati wa utoaji elimu huo, ulioambatana na ufunguaji wa akaunti mbalimbali zilizo chini ya mwamvuli wa WAJIBU, Meneja wa benki hiyo, Tawi la Oyster Plaza, Hildegard Mung'ong'o, alisema elimu waliyopewa watoto waliohudhuria zaidi ya 25 ililenga kuwajengea utamaduni endelevu wa kuweka akiba tangu wakiwa watoto.

Mung'ong'o alibainisha kuwa tawi lake pamoja na matawi 226 yalio sambaa Tanzania yanajiskia fahari kukutanisha watoto na kuwafunza juu ya nidhamu ya fedha na uwekaji akiba kupitia huduma ya WAJIBU inayojumuisha akaunti tatu za Mtoto Akaunti, Chipukizi Akaunti na Mwanachuo Akaunti.

Alisema, benki hiyo kote nchini kama mwendelezo wa kihuduma kwa wateja wake, ilijikita katika maboresho mbalimbali kwa kipindi cha mwezi mzima wa huduma kwa wateja na kwa kutambua umuhimu wa kuweka misingi ya kuongeza wateja wa baadaye, wakaamua kuufunga mwezi wa kuwakutanisha watoto hao.

"Kwanini tumeufunga mwezi wa Huduma kwa Wateja kwa kuwakutanisha watoto hawa. Tumefanya hivi kwa sababu tumelenga kufikisha elimu kwa watoto ambao sio tu watakuwa mabalozi wa benki, bali pia wateja wakubwa watarajiwa wa siku za usoni," alisema Mung'ong'o.

Aliwataka wazazi na walezi kujitokeza matawini kufungua akaunti za watoto ambazo licha ya kadi ya benki kuwa nayo mtoto, mzazi atabaki kuwa msimamizi mkuu wa akaunti kwa kutambua miamala inayofanyika.

Meneja Miradi wa Masuala ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), Lilian Kisamba, alisema WAJIBU ni mwamvuli chanya katika ukuaji wa mtoto kielimu na kinidhamu ya fedha, ulioanza tangu mwaka 2016.

"Tangu hapo, WAJIBU kupitia akaunti za Mtoto, Chipukizi na Mwanachuo, umeweza kuwafikia zaidi ya watoto 90,000 kote nchini, ambako NMB tumewajengea utamaduni chanya huku akaunti zao zikiwa chini ya usimamizi wa wazazi," alisema Kisamba.

# Mkurugenzi afagilia wanawake waliogombea

**Na Beatrice Moses**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Beatrice Domini, amewapongeza wanawake waliojitokeza kugombea majimbo yaliyopo kwenye halmashauri hiyo.

Alitoa pongezi hizo juzi, wakati akizungumza na wagombea ubunge katika Jimbo la Ubungo na Kibamba kabla ya matokeo ya kinyang'anyiro hicho cha uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kutangazwa.

"Nipende kuchukua fursa hii kuwapongeza wagombea wote mliojitokeza, lakini kipekee niwapongeze wanawake kwa uthubutu wao katika kugombea nafasi za uongozi," alisema.

Alibainisha kuwa ni hatua nzuri kwa wanawake hao, ambao jumla walikuwa ni 11 kati ya wagombea 31 waliojitokeza kugombea nafasi hiyo.

Dominic pia alitumia nafasi hii kuwahakikisha kuwa halmashauri haina kinyongo na mgombea yoyote wala vyama vya siasa, wakati ambapo kulizuka hali ya kupishana kauli kwenye mchakato wa kampeni, kwa kuwa wao walijikita katika kuzingatia matakwa na kanuni na sheria za uchaguzi.

Zuweza Abdallah, aliyekuwa mgombea wa Jimbo la Kibamba alimshukuru mkurugenzi huyo ambaye ndiye alikuwa msimamizi mkuu wa uchaguzi kwenye majimbo hayo, jinsi alivyowapa ushirikiano mzuri uliowawezesha kufanya kampeni kwa amani.

"Mvua au wakati wa jua hakujali mkurugenzi alikuwa pamoja nasi, ukimhitaji alikuwa anapatikana kwa wakati anasikiliza na kutoa ushauri, tumefanikisha kampeni na uchaguzi kwa amani ambayo ndiyo msingi, sasa maisha yaendelee vizuri hata baada ya matokeo," alisema.



Askofu wa Kanisa la Pentecoste, Sommy Severua, akizungumza kwenye mahafali ya tisa ya Shule ya New Light iliyopo Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Aina mpya ya mbolea yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya YARA Tanzania, inayotengeneza na kusambaza mbolea nchini, imezindua mbolea mpya inayojulikana kama MiCROP ambayo ni mahususi kwa wakulima wa mahindi na mpunga.

Mbolea hiyo mpya ilizinduliwa jijini Dar es Salaam jana, wakati wa Mkutano wa Mwaka wa Wasambazaji wa Bidhaa za YARA.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema MiCROP ni mbolea yenye mchanganyiko wa virutubisho vya Zinc na Sulphur vinavyohitajika kwenye mazao.

"Tunajivunia kuzindua bidhaa hii mpya ya mbolea ambayo itawasaidia wakulima wadogo wa mpunga na mahindi kupata mazao zaidi na kuongeza kipato zaidi na chakula cha kutosha," alisema.

Kwa mujibu wa Odhiambo, mbolea hiyo itazalishwa jijini Dar es Salaam katika Kiwanda cha YARA kilichoko Kurasini.

"Hii ni katika kuiunga serikali mkono katika uchumi wa viwanda kwani safari hii mbolea tunazalisha hapa hapa nchini," alisema.

Alitoa wito kwa wakulima kuchangamkia mbolea hiyo kwa kilimo bora zaidi na kuongeza kuwa mbolea hiyo itasambazwa nchi nzima.

Katika hatua nyingine kampuni ya YARA imefanya mkutano wa mwaka na wasambazaji wake nchi nzima, ambapo pamoja na mambo mengine, ulilenga kufanya tathmini ya mwaka na kuweka mipango madhubuti kwa ajili ya mwaka ujao.

Wakati wa hafla hiyo, wasambazaji waliovuka malengo yao, walitambuliwa na kutunukiwa zawadi na kampuni hiyo.

# Wanafunzi UDSM washinda tuzo shindano TEHAMA Huawei

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI sita wa kitanzania kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wamefuzu kushiriki shindano la Huawei la TEHAMA duniani, baada ya kufanya vizuri katika fainali za mashindano ya TEHAMA ya Kusini mwa Jangwa la Sahara ya Huawei.

Utoaji tuzo kwa washindi ulifanyika mtandaoni Oktoba 29, 2020. Shindano hilo linalenga kutoa jukwaa kwa vijana wenye vipaji kwenye TEHAMA kuonyesha uwezo wao, kushindana na kuwasiliana, kuhimiza utafiti wa TEHAMA, na kusaidia ukuaji wa mfumo thabiti wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Timu 13 zilizoshinda ni timu kutoka Tanzania, Uganda, Nigeria, Afrika Kusini, Kenya, Lesotho, Mauritius, Zambia. Timu hizo zitashindana na timu kutoka mabara mengine ikiwamo Marekani katika mashindano ya dunia mwezi huu. Miongoni mwa timu zilizopewa tuzo kwenye hafla hiyo ni timu 10 zilizoshiriki upande wa Network Track zikiwamo timu kutoka Tanzania, Uganda, Nigeria, Afrika Kusini, Kenya na Lesotho. Timu hizo zitaenda kushiriki mashindano ya dunia baada ya kuchuana vikali kupata wawakilishi kwa Kanda ya Kusini mwa Jangwa la Sahara. Timu za Nigeria, Mauritius na Zambia zenyewe zilishinda upande wa Cloud Track.

Timu ya Tanzania ilikuwa na wanafunzi 9 ambao waligawanyishwa katika timu tatu. Timu mbili kati ya hizo zimefanikiwa kufika kwenye fainali za dunia, timu ilifanikiwa kushika nafasi ya kwanza kati ya zaidi ya timu 40 zilizoshiriki, na timu nyingine ilishika nafasi ya 4 na hivyo kupata nafasi ya kushiriki fainali za dunia.

Timu hizo zimeundwa na wanafunzi wa Chuo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (COICT) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Washindi wa nafasi ya kwanza ni Mpoki Abel Mwaisela, Hongo Kelvin na Henry Kihanga na washindi wa pili ni Aghatus Biro, John Lazaro na Elisante Akaro.

Hafla ya utoaji tuzo imeashiria miaka mitano mfululizo ya kushiriki kikamilifu shindano la TEHAMA la Huawei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, shindano hilo limekuwa likivutia zaidi ya wanafunzi 50,000 kutoka nchi 14 za Afrika.

Hafla ya utoaji tuzo ilihudhuriwa na maofisa wa ngazi za juu serikalini, viongozi wa tasnia, na wanafunzi, Makamu wa Rais wa Huawei Afrika Mashariki na Kati, Hou Tao.

Akizungumza kama mwakilishi wa walimu wa Chuo Kikuu, Prof. Funso Falade, Rais wa Jumuiya ya Elimu ya Uhandisi Afrika (AEEA), aligusia changamoto kadhaa dhidi ya mafunzo ya wahandisi barani Afrika kama ufadhili, kuchoka kwa akili, na ushirikiano dhaifu wa vyuo vikuu/tasnia.

Pia alisifu jitihada zinazofanywa na Huawei katika kukabiliana na changamoto hizi.

"Fursa za kukuza ujuzi zinazotolewa na Kampuni ya Huawei zinaambatana na lengo na matarajio ya AEEA kwa wanafunzi wetu na eneo muhimu, ambapo sasa tunahitaji utaalamu mwingi barani Afrika kuliko wakati wowote kabla, hasa ukizingatia changamoto zilizoletwa na janga la COVID-19 kwenye mfumo wetu wa elimu," aliongeza.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA 8 WALIOSHINDA MATAJI MENGI LIGI YA MABINGWA ULAYA UK. 12&13



# NYOTA WA5 WANAOMALIZA MIKATABA MWAKA 2021

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili limeshafungwa, lakini uvumi unaendelea kuhusu wachezaji katika usajili wa kipindi cha majira ya joto cha mwakani.

Kuna wachezaji ambao wanamaliza mikataba yao na watakuwa huru kuzungumza na klabu zinazowataka kuanzia Januari Mosi mwakani.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao mikataba yao inamalizika mwishoni mwa msimu huu, hawa hapa...

**#.5 Memphis Depay**

Baada ya kushindwa kukamilisha usajili wake wa kutua katika klabu ya ndoto yake ya Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita, Depay anaonekana kwamba yupo tayari kuondoka pale Lyon ama Januari au kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Ameripotiwa kwamba ameshafikia makubaliano binafsi na miamba hao wa Catalunya na kwamba ana uwezekano mkubwa wa kutua kule.

Kocha wa sasa wa Barcelona, Ronald Koeman, ameshafanya kazi na Depay wakati akiwa anainoa timu ya Taifa ya Uholanzi na ameonyesha wazi kwamba anataka kumchukua nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 akacheze pale Camp Nou.

Zaidi ni kwamba kushindwa kwa Lyon kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, halitakuwa jambo la kushangaza kuona Depay akitua kule Barcelona Januari.

**#4. Mesut Ozil**

Kwa sasa hayupo katika kikosi cha kocha, Mikel Arteta na mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Na ni wazi kwama Ozil ni mmoja wa wachezaji ambao wataondoka kwa 'Washikabunduki' hao mara mkataba wake utakapomalizika. Mchezo wake wa mwisho kuichezea timu hiyo ulikuwa Machi 7, mwaka huu.

Mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki umekuwa mzigo mkubwa kwa Arsenal.

**#3. David Alaba**

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 28 raia wa Austria, ni mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani kwa sasa. Ana ofa nyingi kutoka klabu za Ulaya na yupo kwenye kiwango cha kuvutia zaidi.

Mahusiano kati ya Bayern na Alaba si mazuri kwa wakati huu baada ya rais wa zamani wa Bayern, Uli-Hoeness kumshutumu wakala wa Alaba, Pini Zahavi kwamba anapenda sana fedha. Alaba anatajwa kuwaniwa na Barcelona na Real Madrid.

**#2. Sergio Aguero**

Raia huyu wa Argentina ametumia zaidi ya muongo mmoja pale Manchester City na ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo hadi sasa. Katika umri wake wa miaka 32, ni wazi kwamba itakuwa ngumu kuongezewa mkataba na ana nafasi kubwa ya kuondoka katika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Aguero anatajwa kwamba ataondoka mara tu mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

**#1. Lionel Messi**

Ishu ya Messi ndio ilikuwa habari ya mjini kipindi cha majira ya joto kilichopita na inaonekana wazi kwamba mambo hayajaisha bado. Ilikuwa wazi kwamba alitaka kuondoka Barcelona, klabu ambayo ameitumikia kwa zaidi ya miongo miwili sasa na mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Anahusishwa sana na kwenda kule Manchester City kuungana na kocha wake wa zamani wa Barcelona, Pep Guardiola. Ingawa pia klabu za Inter Milan na PSG zimekuwa zikihusishwa naye, lakini ni wazi kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba hatakuwapo kwa miamba hao wa Catalunya kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

## ISIKUPITE

WAYNE Rooney ndiye mchezaji ambaye anaongoza kwa kuifunga Arsenal mara nyingi zaidi akiwa ameifunga mabao 12 peke yake, kwa sasa anafuatiwa na Jamie Vardy wa Leicester City aliyefanya hivyo mara 11, katika michezo 12 aliyocheza dhidi ya 'Washikabunduki' hao.



## Extra Time




Zinedine Zidane

# MAKOCHA 8 WALIOSHINDA MATAJI MENGI LIGI YA MABINGWA ULAYA

**LONDON, England**

LIGI ya Mabingwa Ulaya ndio mashindano makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya. Zamani michuano hii ilikuwa ikiitwa Klabu Bingwa Ulaya, na ikabadilishwa muundo wake msimu wa 1992-93 na kuitwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Makocha wengi magwiji wameziongoza timu nyingi kwenye mashindano haya. Makocha watano tofauti wameweza kuongoza timu katika mechi zaidi ya 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku mmoja tu akishinda taji hilo kati yao.

Makocha 18 tofauti wameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha miongo mitatu, huku nane tu wakifanikiwa kushinda zaidi ya mara moja.

Makala haya inawachambua makocha nane ambao wana mafanikio zaidi kwenye mashindano haya na wameshinda mara nyingi zaidi taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wafahamu sasa...

### # 8. Ottmar Hitzfeld – Mara 2

Ottmar Hitzfeld alikuwa kocha wa kwanza kushinda mara mbili taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu mbili tofauti akifanya hivyo kwa Bayern Munich mwaka 2001, miaka minne baada ya kuipa Borussia Dortmund taji hilo.

Kwa kipindi chake cha ukocha, Hitzfeld mwenye umri wa miaka 71, alikuwa mmoja wa makocha mwenye mafanikio makubwa zaidi katika soka la Ujerumani.

Mwaka mmoja baada ya kupoteza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa Juventus mwaka 1996, vijana wa Hitzfeld walipindua meza na kuwafunga ya 'Bianconeri' hao wakati Borussia Dortmund walipolitwaa taji hilo mwaka uliofuata.

Miaka miwili baadaye Hitzfeld wakati huo akiwa na Bayern Munich, alitinga fainali, lakini akafungwa na Manchester United wakifungwa mabao mawili dakika za majeruhi katika fainali iliyofanyika jijini Barcelona. Hata hivyo, mwaka 2001 Bayern na Hitzfeld wakalibeba taji hilo.

Changamoto ya mikwaju ya penalti dhidi ya Valencia ikawawezesha 'Bavaria' hao kulibeba taji hilo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1975/76 na likiwa na pili kwa kocha huyo.

### # 7. Jose Mourinho – Mara 2

Ilikuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ambako Jose Mourinho kwa mara ya kwanza alitangaza jina lake barani Ulaya. Wakati huo akiwa na umri wa miaka 41 raia huyo wa Ureno aliiwezesha Porto kuiangusha Manchester United na kubeba taji hilo mwaka 2004 na ndio ukawa mwanzo wa safari ndefu ya mafanikio kwa Mourinho.

Mourinho, ambaye kwa sasa ni kocha wa Tottenham Hotspur, hayupo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu huu 2020-21 kwa sababu Spurs hawakufuzu. Hata hivyo, ameziongoza timu sita tofauti katika mechi 150 katika misimu tofauti 17 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akiwa na Inter Milan mwaka 2010, Mourinho alishinda taji hilo kwa mara ya pili na kuingiza kwenye orodha ya makocha wenye mafanikio makubwa na mashindano hayo. Hata hivyo, tangu hapo hajawahi kutinga fainali ya mashindano hayo.

### #6. Sir Alex Ferguson - Mara 2

Mmoja wa makocha wanaoheshimika kwenye mchezo wa soka duniani, Sir Alex Ferguson ambaye ameshinda mara mbili taji hilo kwa kipindi cha karibia miongo minne ya kuwa kocha.

Miaka tisa baada ya kushinda taji hilo na Manchester United mwaka 1999, raia huyo wa Scotland alishinda taji hilo kwa mara ya pili kwa kuifunga Chelsea kwenye fainali jijini Moscow. Ferguson wakati akishinda taji hilo kwa mara ya pili aliweka rekodi ya kuwa kocha mwenye umri mkubwa zaidi kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya rekodi hiyo kuvunjwa miaka mitano baadaye.

Ferguson kwa misimu 19, ameiongoza timu hiyo katika mechi 194 za Ligi ya Mabingwa Ulaya zikiwa ni nyingi zaidi kuliko kocha mwingine yeyote.

### # 5. Vicente Del Bosque – Mara 2

Vicente Del Bosque ni mmoja wa makocha wenye historia nzuri kwenye mchezo wa soka. Kocha huyo mwenye umri wa miaka 69 raia wa Hispania ndiye kocha pekee kushinda Kombe la Dunia, Kombe la Mataifa ya Ulaya (Euro) na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kabla ya kuwa na mafanikio kwenye soka la kimataifa, Del Bosque alijenga jina lake kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid ambako alishinda mara mbili taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Fainali ya msimu wa 1999-2000, ambapo ilikuwa mara ya kwanza kuzikutanisha timu za nchi moja kwenye fainaliya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid ilifunga mara tatu dhidi ya Valencia na kushinda taji lao la pili la mashindano hayo ndani ya miaka mitatu na la nane kwao.

Na ndio lilikuwa taji lake la kwanza la mashindano hayo kwa kocha, Del Bosque. Miaka miwili baadaye, Zinedine Zidane alifunga bao zuri dhidi ya Bayer Leverkusen mjini Glasgow kuipa taji la tisa la mashindano hayo, Real Madrid huku Del Bosque akilibeba kwa mara ya pili.

### # 4. Pep Guardiola – Mara 2

Pep Guardiola ni mmoja wa makocha bora zaidi kwa kizazi cha sasa. Alitengeneza jina lake akiwa na Barcelona ambako alikuwa na mafanikio makubwa zaidi.

Wakati wa kipindi chake pale, Guardiola akiwa na wakali kama Lionel Messi, Andres Iniesta na Xavi Hernandez, alishinda mara mbili taji hilo kwa kipindi cha miaka mitatu. Kwa mara ya kwanza alishinda mwaka 2009.

Akashinda kwa mara ya pili mwaka 2011 kabla ya kuondoka Barcelona kwenda Bayern Munich na baadaye Manchester City.

Februari mwaka huu, Guardiola aliweka rekodi ya kushinda mechi nyingi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wakati Man City walipoitoa Real Madrid hatua ya mtoano ya timu 16.

### # 3. Jupp Heynckes – Mara 2

Jupp Heynckes alitengeneza jina lake kule Real Madrid wakati alipoibebesha taji la Ligi ya Mabingwa mwaka 1998, ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 32 waliposhinda kwa mara ya mwisho taji hilo ikiwa ni kwa mara ya sita.

Muongo mmoja na nusu baadaye, raia huyo wa Ujerumani akawa kocha mwenye umri mkubwa zaidi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Bayern Munich.

Katika kipindi chake pale Bayern Munich, Heynckes alikuwa kocha wa kwanza kushinda mechi 11 mfululizo katika mashindano hayo.

### # 2. Carlo Ancelotti – Mara 3

Baada ya kushinda mara mbili taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na miamba wa soka la Italia, AC Milan, Carlo Ancelotti alielekea Real Madrid ambako aliwapa taji hilo mwaka 2014.

Tangu waliposhinda taji lao la tisa katika mashindano hayo mwaka 2002, Real Madrid haikuweza kutinga fainali kwa kipindi cha miaka 12 kabla ya kufanya hivyo mwaka 2014 kwa kukutana na wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid.

Baada ya Sergio Ramos kufunga katika muda wa ziada, Cristiano Ronaldo akawa mchezaji wa kwanza kufunga kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa timu mbili tofauti wakati Los Blancos wakilibeba taji hilo kwa mara ya kumi.

Na hiyo ikamfanya kocha huyo wa Italia ambaye ameziongoza timu katika mechi 165 za mashindano hayo katika misimu 18 tofauti, kushinda taji hilo kwa mara ya tatu akiwa kocha.

Licha ya AC Milan na Real Madrid, Ancelotti pia amezinoa timu kama Parma, Juventus, Chelsea, Paris St. Germain, Bayern Munich, na hivi karibuni Napoli kwenye mashindano hayo.

### # 1. Zinedine Zidane – Mara 3

Baada ya kipindi cha uchezaji wa mafanikio, Zinedine Zidane mafanikio yake yakahamia pia kwenye ukocha.

Mfaransa huyo alishinda taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa kocha mwaka 2016, ambapo ilimfanya kuwa mtu wa kwanza baada ya Pep Guardiola kushinda taji hilo akiwa mchezaji na baadaye kocha.

Zinedine akalitwaa taji hilo kwa mara ya pili mwaka 2017 kabla ya kulibeba tena mwaka 2018 na kuweka historia ya kushinda taji hilo mara ya tatu mfululizo na kufikia idadi sawa na Ancelotti, ambapo hadi sasa ndio makocha pekee walioshinda taji hilo mara tatu katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## Nukuu

"Nimewanoa mabingwa wakati nikiwa kocha, kutoka (Oliver) Bierhoff hadi (George) Weah na Adriano, lakini najutia sikuwahi kumnoa [Zlatan] Ibrahimovic, yeye ni mchezaji wa daraja la juu kabisa, na sielewi kwa nini hajawahi kushinda tuzo ya Ballon d'Or. Nchini Italia, ameweka uwiano zaidi kuliko [Cristiano] Ronaldo. Ni jambo la wazi tangu ujio wake, wachezaji vijana wamehamasika naye zaidi kuliko Ronaldo," **Kocha wa zamani wa AC Milan na Juventus, Alberto Zaccheroni**



"Ni wazi kwamba, sasa safari yake [Kylian Mbappe] ni Liverpool, anaonyesha hana nia ya kwenda Real Madrid," **gazeti la Le Parisien likimnukuu mtu wa karibu na Mbappe.**



"Nadhani huu ni wakati wa kutumia mabeki wanne. Nimekuwa nikisema hili tangu mwanzo wa msimu, natarajia atabadilika kwenye mchezo ujao, kwa sababu hilo hata yeye atakuwa ameliona, walinzi watatu nyuma ni mfumo mbaya ukikutana na timu inayoshambulia zaidi kama ilivyotokea kwa Manchester City," **Nahodha wa zamani wa Arsenal, Tony Adams, akimtaka Mikel Arteta kutumia mfumo wa mabeki wa tatu.**



# SIMBA ILIVYOIUA MWADUI KWA SHOO YA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

IMEZOELEKA kwa timu kubwa za Simba, Yanga na hata Azam kubebwa zaidi na wachezaji kutoka nje ya nchi. Jumamosi iliyopita bao pekee la ushindi la Yanga lilifungwa na Mghana Michael Sarpong dhidi ya Biashara United, linaifanya timu hiyo kuendelea kubebwa zaidi na wachezaji kutoka nje ya nchi kwani katika mabao yao tisa iliyofunga, manane yamefungwa na wachezaji wa kigeni.

Ni bao moja tu la Yanga lililofungwa na mchezaji wa Kitanzania ambaye ni Waziri Junior kwenye mechi dhidi ya KMC, Yanga ikishinda 2-1.

Ukiondoa Sarpong, wengine walioifungia mabao Yanga ni Carlos Carlinhos raia wa Angola, Tonombe Mukoko na Tuisila Kisinda wote raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Lamine Moro raia wa Ghana, Sogne Yacouba raia wa Burkina Faso na Mnyarwanda Haruna Niyonzima.

Kwa upande wa Azam, wanaoibeba zaidi ni wachezaji Prince Dube kutoka Zimbabwe, Mzambia Obrey Chirwa, wakisaidiwa na Richard Djodi kutoka Ivory Coast.

Kikosi cha Simba chenyewe kinabebwa zaidi na Mnyarwanda Meddie Kagere, Mkongomani Chris Mugalu, Clatous Chama raia wa Zambia, Luis Miquissone raia wa Msumbiji ambao ndio wafungaji wao mengi.

Kwenye mechi ya Jumamosi kati ya Simba dhidi ya Mwadui mambo yalibadilika. Shoo ya kibabe ya wachezaji wa Kitanzania iliwamaliza kabisa Mwadui FC na kusababisha kupokea kipigo cha mabao 5-0.

Kwa muda mrefu haijawahi kutokea kwenye timu ya Simba kufunga idadi ya kuanzia mabao matatu asiwapo mchezaji yeyote wa kigeni. Hii ni tangu enzi za kina Emmanuel Okwi, Felix Sunzu na hayati Patrick Mafisango.

Kilichotokea Jumamosi ni rekodi ya aina yake, kwani mabao yote matano yamefungwa na wachezaji wa Kitanzania watupu.

Na hii ni baada ya Simba kupokea vipigo viwili vya bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons na kipigo kama hicho kutoka kwa Ruvu Shooting.

Simba ilirudi kwa hasira na kushinda mabao 5-0, huku wachezaji wa Kibongo wakitamba kwenye mechi hiyo...

John Bocco

Nahodha wa Simba, Bocco alifunga bao la kwanza dakika ya 25.



Hassan Dilunga na Ibrahimu Ajibu wakishangilia kwa furaha baada ya kuifungia timu hiyo, huku Hamisi Ndemla (kushoto), akiwakimbilia kuungana nao wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mwadui FC iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Mbongo huyo alifunga bao hilo ingawa msaada mkubwa ulikuwa kwa wachezaji wawili wa kigeni, Chama aliyeondoka na mpira na kumpasia Miquissone ambaye alimrudishia Chama, aliyempasia mfungaji akaukwamisha wavuni kirahisi.

Bocco alifunga bao la pili dakika ya 64 na hili lilitengenezwa na Watanzania watupu, kwani Hassan Dilunga, mchezaji aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Larry Bwalya, aliambaa na mpira kwenye winga ya kulia na kupiga krosi ya chini iliyomkuta mfungaji akaukwamisha wavuni.

Ibrahim Ajibu

Aliingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Bocco. Ilikuwa ni dakika ya 81, alipofunga bao la tatu, likiwa ni la kwanza kwake msimu huu.

Ajibu akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, alipokea pasi ya kichwa kutoka kwa Mbongo mwenzake, Dilunga. Alichokifanya ni kunyoosha mguu na kuachia shuti kali lililokwenda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa wa Mwadui Mussa Mbisa akichupa bila mafanikio.

Hassan Dilunga

Ilikuwa ni shoo la Ndemla na Dilunga. Katikati ya uwanja, Ndemla aliupata mpira ulioonekana kuwa hauna madhara. Inawezekana Mwadui walikariri kuwa Simba inapiga pasi fupi fupi. Ndemla alinyanyua macho na kupiga pasi ndefu ya juu, iliyomkuta Dilunga ambaye alifukuzana na Gerald Mgeveke, aliyemzidi mbio na nguvu kabla ya kuujaza wavuni dakika ya 86 na kuwa bao la nne kwenye mchezo huo. Lilikuwa ni bao lake la kwanza msimu huu, huku tayari akiwa na pasi mbili zilizozaa mabao kwenye mechi hiyo.

Hamisi Ndemla

Ilikuwa ni ndani ya dakika tisa tu, Simba ikifunga mabao matatu, kwani dakika ya 90 bao la tano lilipatikana.

Baada ya kutoa pasi ya bao la nne, Ndemla naye alitafuta la kwake. Alichukua mpira katikati ya uwanja na kuanza kupiga chenga za hapa na pale taratibu na ilionekana kwa mabeki wa Mwadui kama vile anataka kutoa pasi, lakini alikuwa akisonga mbele. Alipofika kiasi cha mita 30 aliachia fataki la chini chini na mpira ukajaa wavuni kuandika bao tano kwa Simba, huku likiwa la kwanza kwake kwa msimu huu.

## JE, WAJUA?



SAMUEL Eto'o ndiye mchezaji aliyeshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili mfululizo akiwa na timu mbili tofauti. Pia ni mchezaji pekee kushinda Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia mara mbili mfululizo akiwa na klabu mbili tofauti Barcelona msimu wa 2008-09 na Inter Milan msimu uliofuata.



# Mashamba darasa yaanzishwa Mpwapwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, ameagiza kuanzishwa kwa mashamba darasa kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya, sokoni na ofisi za kijiji, ili wananchi wapate ujuzi kuandaa bustani kwa ajili ya vyakula vyenye virutubishi muhimu.

Shekimweri aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wilayani humo kwenye kikao cha idara mtambuka zinazohusika moja kwa moja na masuala ya lishe kwenye halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema kuwa kuanzishwa kwa mashamba darasa kutasaidia kupata ujuzi wa namna ya kuandaa bustani au mashamba ya vyakula vyenye virutubishi muhimu kwa afya na ukuaji wa binadamu hususan watoto.

Aidha, aliutaka uongozi wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, suala la utunzaji wa bustani za mboga na upandaji miti isiwe adhabu kwa wanafunzi.

"Suala la upandaji wa miti au utunzaji wa bustani kwa wanafunzi liwe ni shughuli ya kawaida kwao na si adhabu ili watoto baada ya kumaliza masomo wawe na maarifa ya kutekeleza wakiwa nyumbani," alisema.

Alisema lishe bora ni msingi wa afya bora na humjenga binadamu kimwili na kiakili.

Awali, Ofisa Lishe wa Wilaya hiyo, Asiatu Mmbwambo, alisema kwa sasa shughuli za lishe kwenye wilaya hiyo zimependa kutoka asilimia 27 hadi 55.

"Zimependa kutokana na awali halmashauri ilikuwa haitoi fedha zilizotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya shughuli za lishe hivi sasa utekelezaji ni mzuri kwa kuwa halmashauri inatoa fedha kwa ajili hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema hatua hiyo imesaidia wilaya kutoka kwenye alama nyekundu iliyokuwa inaashiria hatari na kupata alama ya njano inayoashiria hali nzuri.

Aidha, alisema malengo ya wilaya hiyo ni kupata alama ya kijani.



Wafanyabiashara wa soko la Sabasaba katika Jiji la Dodoma, wakiwa wamelala kwenye meza za kufanyia biashara ambazo zimesusiwa na hivi sasa zimegeuzwa kuwa sehemu ya kulala kutokana na kutotumika kwa muda mrefu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# H/shauri yataja miradi ya kimkakati ya bil. 215

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetaja miradi ya kimkakati 14 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 215 inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa kupitia mapato ya ndani ili kuongeza mapato.

Pia miongoni mwa miradi hiyo inalenga kutoa huduma kwa wananchi na kupendezesha mji.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili juu ya mikakati ya Jiji hilo kujiimarisha kimapato.

Alisema kwa sasa Jiji hilo linajenga mradi wa 'Government City Complex' katika Mji wa Serikali Mtumba kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 35,152.4.

"Mradi huu una thamani ya Sh. bilioni 59.31 ambapo kwa sasa ujenzi upo awamu ya kwanza kwa gharama ya Sh. bilioni 18.87 na Sh. bilioni 4.1 zimelipwa," alisema.

Aidha, alisema kuna mradi wa ujenzi wa hoteli (Dodoma City Hotel) inayojengwa katikati ya mji kwenye eneo maarufu la 'Paradise cinema hall' ambao una thamani ya Sh. bilioni 9.99 ambazo zinatokana na mapato ya ndani, ambapo hadi sasa Sh. bilioni 3.44 imetumika.

Kadhalika, alisema jiji hilo lina mpango wa kutekeleza miradi mingine mikubwa ya kimkakati ambayo tayari imeshasanifiwa ikiwamo m radi wa Nunge wenye thamani ya Sh. bilioni 5.74.

Alitaja mingine ni City Complex Apartment yenye thamani ya Sh. bilioni 20.85, N.K Complex yenye thamani ya Sh. bilioni 31.77, City Complex Mall yenye thamani ya Sh. bilioni 62.17 na Nyerere Square Plaza yenye thamani ya Sh. bilioni 27.

"Pia ujenzi wa mradi wa maji Njedengwa wenye gharama ya Sh. bilioni 1.4, ujenzi wa mradi wa maji Hombolo wenye Sh. milioni 610, ujenzi wa mradi wa maji Chihikwi wenye gharama ya Sh. milioni 90.6," alisema.

Mafuru alisema pia halmashauri imefanikiwa kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa miradi. "Jiji limetekeleza ujenzi wa miradi ya vituo vya afya Makole, Mkonze, Hombolo, pia limefanikiwa ujenzi wa masoko ya Kikuyu, Chadulu na Bonanza, pia kuboresha minada ya Mpunguzi na Msalato," alisema.

# Sababu shughuli uchumi kupaa jijini Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kutokana na serikali kuhamia Dodoma kumekuwapo na ongezeko kubwa la shughuli za kiuchumi na kijamii, hivyo kuchangia uhitaji wa usafiri wa anga.

Aidha, watumishi 17,080 tayari wamehamia na serikali inafanya kazi zake Dodoma.

Katibu wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuratibu Serikali kuhamia Dodoma, Meshack Bandawe, aliyasema hayo juzi baada ya kuwasili kwa ndege ya Airbus ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa mara ya kwanza jijini hapa.

Alisema kutokana na ongezeko la shughuli hizo, serikali imeendelea na jitihada za kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara na usafiri wa anga.

"Zipo barabara nyingi zimejengwa, kwa sasa Tanroards wana mpango wa kupanua barabara ya Dodoma hadi Chamwino itakayoenda sambamba na ukarabati wa barabara ya Morogoro hadi Dodoma, kuna ujenzi wa barabara za mizunguko ya nje kilometa 110, barabara ya mizunguko ya ndani kilometa 39.5," alisema.

Bandawe alisema Shirika la Ndege limeona kuwapo kwa fursa ya ongezeko la shughuli hizo hatua inayosaidia utekelezaji wa azma ya serikali kuhamia Dodoma.

"Walianza safari za ndege kwa kuja mara tatu kwa wiki, lakini wakabadili sasa zinakuja kila siku kwa kutumia Bombadier, hivyo pamoja na bombardier kuja kila siku sasa na Airbus hii itaanza kuja Dodoma, ni jambo la kupongeza sana," alisema.

Kadhalika, alisema ujenzi wa miji wa serikali unaendelea kutekelezwa kwa kasi ambapo ujenzi kwa awamu ya kwanza majengo 23 ya wizara yamekamilika.

"Muda si mrefu tunaanza ujenzi wa majengo mengine lengo ni kuboresha majengo ya ofisi, pia ujenzi wa ofisi za taasisi unaendelea," alisema.

Katibu huyo alisema katika uboreshaji wa usafiri wa anga, uwanja wa Dodoma umepanuliwa, takribani Sh. bilioni 11 zimetumika kulipa fidia kwa wananchi ili kupisha eneo hilo.





# Mbunge mteule Mbarali atoa neno

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MBUNGE mteule wa Jimbo la Mbarali lililoko mkoani Mbeya, Francis Mtega, amewaomba wananchi waote wa jimbo hilo, bila kujali itikadi za vyama vya kisiasa kushirikiana kwa pamoja katika kuleta maendeleo ndani ya jimbo hilo.

Aliyasema hayo juzi wakati akitoa shukrani kwa wananchi wa Mbarali kumchagua kwa mbunge wa jimbo hilo kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kupata kura 55,737 akimshinda mpinzani wake Liberatus Mwang'ombe wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) aliyepata kura 28,104 kati ya kura 87,548 zilizopigwa.

Mtega alisema ana imani hata vyama vya upinzani vilimpigia kura ndio maana kapata ushindi huo, na kwamba kazi kubwa sasa ni kuhakikisha Wanambarali wanapata maendeleo.

"Nitaenda kushughulikia suala la migogoro kati ya wafugaji na wakulima, tutahakikisha tunatenga maeneo maalum kwa ajili ya josho na malisho tutatunga sheria ndogo za kudhibiti wafugaji wanaoingiza mifugo kwenye mashamba. Lakini tutaendelea kutoa elimu ya kuzuia wafugaji kutoingiza mifugo kwenye hifadhi zetu za Taifa hususani ya Ruaha," alisema Mtega.

Aliwahimiza vijana na wanawake kuendelea kujiunga kwenye vikundi ili kupata mikopo ya halmashauri ambayo hutolewa kwa masharti nafuu, na kwamba atahakikisha kupitia mfuko wa jimbo anatoa fursa ya mikopo pia.

Katibu Mwenezi wa CCM wilayani humo, Kassim Kondo, alisema chama chao kitasimamia na kutekeleza Ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025 katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema ndani ya Ilani hiyo Wilaya ya Mbarali yamo, ambapo yameelezwa masuala mbalimbali ambayo yatatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia sekta ya kilimo, afya, maji, miundombinu ya barabara na elimu kwa kuhakikisha yanatengenezwa mazingira rafiki kwa maslahi ya wananchi.

Alisema moja ya masuala ya kufurahisha katika Ilani hiyo ni serikali kusimamia kikamilifu suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa kuhakikisha wakulima wa mpunga wanapata mbolea za kupandia na kukuzia kwa wakati pamoja na kupunguza baadhi ya tozo na ushuru wakati wa kusafirisha mazao shambani, lakini kuwadhibiti wafanyabiashara walanguzi.

Aliongeza kuwa pia serikali imewahakikishia soko la uhakika wakulima wa mpunga ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha vituo maalumu vya kuuzia mchele kwa kuanzia sasa kipo Kata ya Igurusi.

# RC awakumbusha watumishi kutimiza wajibu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaomba viongozi na watumishi wa halmashauri na wilaya zote za mkoa huo, kutimiza wajibu wao ipasavyo katika kuwatumikia wananchi ili kuwaletea maendeleo.

Chalamila alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe juu ya masuala wanayopaswa kuzingatia watumishi wa umma baada ya uchaguzi kumalizika. Alisema watumishi na viongozi wa serikali wako kwa ajili ya kuwatumikia wananchi kwa lengo la kuwaletea maendeleo, hivyo wanapaswa kuwa wazalendo na wenye mienendo inayopendeza kwa jamii.

"Ni wakati sasa wa kuchapa kazi tuache maneno au makundi kwa sababu yatatupotezea muda, twende tukateleze na kusimamia miradi ya maendeleo kwa wananchi... sitakubali kuona mtumishi aliyeaminiwa anakuwa kikwazo huyo hatatufaa," alisema Chalamila.

Katika hatua nyingine Chalamila alipongeza kasi ya ujenzi wa ofisi mpya ya mkoa huo kwa maelezo ni ya kuridhisha na kwamba jengo hilo ni kubwa na la mfano nchini.

Alisema kiasi cha shilingi bilioni mbili kitatumika kukamilisha jengo hilo ambalo litakuwa la ghorofa tano, na kwamba litakuwa na huduma zote muhimu pamoja na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Alimwomba mkandarasi anayesimamia jengo hilo, Mhandisi Lupakisyo George, kukamilisha mradi huo kwa wakati kama walivyokubaliana kwenye mkataba.

Mhandisi Lupakisyo alimwahidi Mkuu wa Mkoa huo, kwamba ndani ya kipindi cha miezi 12 utakuwa umekamilika.

Alisema waliamua kukamilisha ndani ya kipindi cha miezi 12 badala ya 18 kama walivyokubaliana kwenye mkataba kutokana na kasi waliyonayo ya ujenzi ambapo hufanya kazi usiku na mchana.

"Mradi huu tulianza Juni mwaka huu, ambapo hadi sasa umefikia asilimia 30 kwa mwendo huu tunatamani mpaka kufika Juni 2021 ujenzi utakuwa umekamilika," alisema Mhandisi Lupakisyo.

Mmoja wa kinamama, Beatrice Mwaipyana ambaye ni miongoni mwa waliopata ajira katika mradi huo, alisema umesaidia kupata fedha za kuendesha maisha yao ya kila siku.



Wataalamu wa utafiti wa kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, wakikagua shamba la maharage ambalo limepandwa kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za zao hilo. zitakazosambazwa kwa wakulima. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakulima tumbaku wataka utabiri wa hali ya hewa kabla ya msimu

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

CHAMA Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku (CHUTCU) katika Halmashuari ya Wilaya ya Chunya, kimewaomba watabiri wa hali ya hewa kutoa utabiri mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza, ili kufahamu ni wakati gani mzuri kwao kwa ajili ya kilimo cha tumbaku.

Ombi hilo limetolewa na Kaimu Meneja wa chama hicho, Juma Nshishi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema mara kadhaa wamekuwa wakipata mavuno hafifu kutokana na kutopata taarifa sahihi za hali ya hewa. Alisema wataalamu wa hali ya hewa wanapaswa sasa kutoa taarifa mapema juu ya utabiri kwa miezi mitatu au minne ijayo kwa ajili ya kusaidia wakulima kufanya maandalizi mapema ya kulima.

"Moja ya maeneo yanayosababisha wakulima kupata mavuno kidogo ni kwenye masuala ya hali ya hewa, hili eneo halijatoa bado elimu ya kutosha kwa wakulima... ombi letu ni kwamba watusaidie wakulima kutupa ripoti za mara kwa mara itasaidia kufahamu upi ni wakati sahihi wa kuanza maandalizi ya kilimo," alisema Nshishi.

Alisema hali ya hewa msimu wa kilimo 2018/2019 ulikuwa mbaya kutokana na mvua kuwa nyingi na kuharibu zao la tumbaku mashambani.

"Msimu uliopita wakulima wetu walipata hasara kubwa sana kwa kuwa walitumia gharama kubwa za pembejeo za kilimo kama mbolea zilizosombwa na maji kutokana na mvua nyingi kunyesha," alisema Nshinshi.

Salome Kilasi, miongoni mwa wakulima wa tumbaku, aliiomba serikali msimu ujao wa kilimo iongeze nguvu kwa kuhakikisha wakulima wanafikiwa na pembejeo za kilimo kwa wakati, ikiwamo kuwabana mawakala wanaouza pembejeo feki.

Alisema eneo hilo la pembejeo feki nalo likidhibitiwa basi wakulima wataweza kuzalisha mazao mengi kwani tayari wakapewa taarifa sahihi za hali ya hewa pamoja na usalama wa pembejeo watakazozitumia.

# Leo siku ya mapumziko Z'bar, Mwinyi kuapishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ametangaza kwamba siku ya leo itakuwa siku ya mapumziko.

Dk. Shein amefanya uamuzi huo ili kutoa fursa kwa watumishi wa umma na wananchi kuhudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais mteule wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa Rais wa Zanzibar, sherehe hizo zitafanyika viwanja vya Amani Mjini Unguja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotiwa saini na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Abadulhamid Yahya, tangazo hilo amelitoa kwa uwezo aliopewa chini ya Kifungu cha 6(1) (a) cha Sheria ya Mambo ya Rais Nambari tatu ya mwaka 2020.

Dk. mwinyi alitangazwa mshindi Oktoba 29, mwaka huu na Tume ya Uchaguzi Zanzibar baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa Oktoba 28 na kupata kura 380,402 sawa na asilimia 76 na kumshinda mpinzani wake, Maalim Seif Sharif Hamad wa ACT- Wazalendo aliyepata kura, 99,103 sawa na asilimia 19.87.

Katika kinyang'anyiro hicho wagombea 17 walishiriki uchaguzi huo, mgombea wa Chama cha ADA-TADEA aliyepata kura 392 sawa na asilimia 0.08, Hamadi Rahid Muhammed wa ADC alipata kura 996 sawa na asilimia 0.20, Muhammed Omar Shaame wa UMD alipata kura 104 sawa na asilimia 0.02 na Hamad Muhammed Ibrahim wa UPDP alipata kura 181 sawa na asilimia 0.04.

Wengine ni Othman Khamis wa CCK aliyepata kura 2,235 sawa na asilimia 0.45, Said Issa Muhammed wa CHADEMA aliyepata kura 1,702 sawa na asilimia 0.34, Ali Omar Juma wa CHAUMA aliyepata kura 249 sawa na asilimia 0.05, Mussa Haji Kombo wa CUF aliyepata kura 1428 sawa na asilimia 0.29.

Wengine ni Shafi Hassan Suleiman wa DP aliyepata kura 106 sawa na asilimia 0.02, Ameri Hassan Ameri wa DM aliyepata kura 133 sawa na asilimia 0.03, Khamis Faki Mgau wa NRA aliyepata kura 160 sawa na asilima 0.03, Mfamau Khamis Hassan wa NLD aliyepata kura 122 sawa na asilimia 0.02, Issa Muhamed Zonga wa SAU aliyepata kura 102 sawa na asilimia 0.02, na Hussein Juma Salum wa TLP aliyepata kura 142 sawa na asilimia 0.03.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya YARA Tanzania, Winstone Odhiambo (kulia), akiwaelekeza jambo wasambazaji wa bidhaa za kampuni hiyo, wakati wa uzinduzi wa mbolea ya MiCROP wakati wa mkutano wa mwaka wa wasambazaji jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii 530 wawasili kutoka Russia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATALII 531 wamewasili juzi katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume wakitokea nchini Russia.

Ujio huo ni historia kwa Zanzibar ya kupata ndege ikiwa na idadi kubwa ya watalii kama hiyo tangu kuanzishwa kwa viwanja vya ndege.

Watalii hao waliwasili kwa Shirika la Ndege la Azur Air kutoka Urusi ikiwa na watalii wenye rika tofauti ambao wengi wao ni vijana. Akizungumza baada ya kuwasili kwa ndege hiyo, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdallah Muhammed Juma, alisema licha ya ujio wa wageni hao, lakini Zanzibar inatarajia kupokea ndege 100 za watalii ambazo zipo katika foleni ya kuja Zanzibar.

"Ndani ya miezi sita ijayo kuanzia Desemba mwaka huu ndege 100 zimeshaweka foleni ya kuja Zanzibar, ambazo zinatoka katika masoko mapya ya Ulaya Mashariki," alisema Dk. Juma.

Alisema baada ya Tanzania kufanikisha kutokomeza ugonjwa wa corona, utalii umefunguka na hoteli nyingi sasa zitafunguliwa kutokana na watalii wengi kuwasili Zanzibar.

"Zanzibar njema atakaye aje... niwaambie vijana wale ambao ajira zao zilisitishwa hotelini kutokana na kufungwa baada ya kukosa wageni kutokana na janga la corona, sasa vijana wajiandae kufanya kazi maana idadi kubwa ya watalii watamiminika Zanzibar," alisema.

Alisema ujio huo wa wageni kwa kiwango kikubwa hoteli nyingi zitafunguliwa na ajira mpya zitapatikana, hivyo maisha ya wananchi waliokuwa wakitegemea utalii sasa watayarishe bidhaa zao.

Alieleza kuwa licha ya kupokea ndege hiyo, pia nyingine nne kubwa zilileta wageni mwishoni mwa wiki iliyopita kutoka masoko mapya ya utalii ambayo ni Russia, Ukraine na Kazathtan.

Alieleza kuwa awali Zanzibar ilikuwa inategemea masoko ya utalii ya zamani ambayo ni Italia, Ufaransa, Uingereza, Marekani na Ujerumani.

Alieleza kuwa wakati dunia imepumzika kusafirisha wageni kwa sababu ya corona, Kamisheni ya Utalii Zanzibar ilikuwa ikifanya kazi kubwa ya kuitangaza Zanzibar kiutalii, hivyo baada ya corona kumalizika, matunda sasa yameanza kuonekana kutokana na ujio wa watalii hao.

Alisema wameshazungumza na jumuiya ya wawekezaji kutoka Uturuki, na kuwa wanatarajia kuwasili kwa ndege nyingine mpya ambayo itakuja Novemba 5, mwaka huu ikiwa na watalii zaidi ya 500 kutoka Russia.

# Wanawake 12 waibuka kidedea uwakilishi, ubunge

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE 12 waliogombea ubunge na uwakilishi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, wameshinda katika uchaguzi huo na kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Wanawake hao 11 ni kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mmoja kutoka Chama cha Wananchi (CUF). Wanawake watano ni kutoka majimbo ya Kisiwani Pemba na saba kutoka majimbo ya Unguja.

Wanawake hao ni Harusi Said Suleiman mwakilishi mteule wa Jimbo la Wete Pemba kupitia CCM.

Mwingine ni Mariyam Thani Omar mwakilishi mteule wa Jimbo la Gando Kisiwani Pemba kupitia CCM na Zawadi Amour Nassor mwakilishi mteule kutoka Jimbo la Konde CCM kutoka Pemba.

Mwakilishi mteule mwingine kutoka Kisiwani Pemba ni Bahati Khamis Kombo kutoka CCM Jimbo la Chambani na mgombea mteule nafasi ya ubunge Mariyam.

Kwa upande wa Kisiwani Unguja wanawake wote saba walioshinda ni kutoka CCM na nafasi ya uwakilishi ni wanne na nafasi ya ubunge ni watatu.

Wagombea hao wateule ni Asha Abdallah Mussa uwakilishi Jimbo la Mahonda, Mtumwa Peya, uwakilishi Jimbo la Bubwini, Mwanaasha Khamis Juma Jimbo la Dimani na Rukia Omar Mapuri Uwakilishi Jimbo la Amani. Kwa upande wa nafasi ya ubunge ni Zubeda Khamis Jimbo la Mfenesini aliyepata, Mwantakaje Juma na Mwanakhamis Kassim Said Jimbo la Magomeni.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliwapongeza wanawake hao walioshinda katika kinyang'anyiro hicho.

Alisema ushindi wao huo umechangiwa na kuungwa mkono na wapigakura wanawake na wanaume kwa kuwaamini wagombea hao kuwa viongozi wao.

"Tunawapongeza sana wanawake wote walioshinda katika majimbo ya uchaguzi, kwani wamethubutu na wameonyesha uwezo wao katika kunadi sera zao na kukubalika," alisema.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa ni kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi, Chama cha CUF kupata mbunge mwanamke aliyeshinda katika uchaguzi kwa upande wa Pemba.

# HAFLA YA JPM KUKABIDHIWA CHETI



Rais mteule, Dk. John Magufuli, akiwa amesimama na waliogombea urais kupitia vyama mbalimbali vya upinzani, wakati Wimbo wa Taifa ukipigwa katika hafla fupi ya kukabidhiwa cheti cha ushindi. **PICHA: IKULU**



Rais mteule, Dk. John Magufuli akisalimiana na kiongozi wa jopo la waangalizi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika uchaguzi mkuu, Rais mstaafu wa Burundi, Silvestre Ntibantunganya, baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi wa kiti cha urais, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**




Rais mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, akimpongeza Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi kwa kiti cha urais katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: IKULU**




Kikundi cha ngoma cha Hombolo jijini Dodoma kikitumbuiza wakati wa hafla ya kukabidhi cheti kwa mshindi wa kiti cha urais zilizofanyika jana, eneo la Njedengwa jijini Dodoma. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya waliokuwa wagombea wenza wa urais kwenye uchaguzi mkuu 2020 wakishiriki hafla ya kukabidhi cheti kwa Rais mteule, Dk. John Magufuli, jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Uhuru Kenyatta ampongeza Magufuli

**Nairobi, KENYA**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amempongeza Rais mwenzake wa Tanzania, John Magufuli kwa kushinda uchaguzi mkuu.

Rais Kenyatta alisema kuchaguliwa tena kwa Magufuli ni ishara ya upendo na imani waliyo nayo Watanzania kwa uongozi wake.

"Kwa niaba ya watu, Serikali ya Kenya na mimi mwenyewe nampongeza ndugu yangu, Dk. John Magufuli kwa ushindi wako na wa Chama Cha Mapinduzi, katika uchaguzi uliomalizika," alisema Kenyatta.

"Nchi ya Kenya inatarajia kuendelea kufanya kazi na utawala wako kwa faida ya watu wa mataifa yetu mawili, kwa ustawi wa Afrika Mashariki na kwa amani, outlive na ukuaji wa Bara la Afrika."

Rais Kenyatta pia alimtakia rais mwenzake wa Tanzania afya njema na ufanisi anapojiandaa kuhudumu kwa muhula wa pili madarakani na kumhakikishia ushirikiano wa Kenya na kwa utawala wake.

Rais wa Tanzania, John Magufuli ametetea nafasi yake baada ya kushinda kwa kishindo uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatano.

Magufuli ameshinda kwa kupata kura 12,516,252 ambayo ni asilimia 84 ya kura zote zilizopigwa.

Tundu Lissu kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (upinzani) alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 1,933,271 ya kura zote zilizopigwa.

Jumla ya watu 15,919,500 waliopiga kura hizo wakati waliojiandikisha kupiga kura walikuwa 29,754,699 kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Hata hivyo vyama vikuu vya upinzani wamekataa matokeo ya uchaguzi huo wakidai uligubikwa na udanganyifu.

Uchaguzi huu ambao Magufuli alikuwa akiwania nafasi hiyo ya juu alikuwa na washindani wengine 14.

*BBC*



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta (kushoto) akiwa na Rais John Magufuli, alipofanya ziara binafsi ya siku mbili nchini Tanzania mwaka 2019. **PICHA: STORM FM GEITA**

# Waokoaji waendelea kuwasaka waathirika wa tetemeko Uturuki

**Aegean, UTURUKI**

TIMU za uokozi zinaendelea kutafuta manusura kwenye vifusi vya majengo nane yaliyoanguka mwishoni mwa wiki wakiwasaka walionusurika katika tetemeko kubwa la ardhi nchini Uturuki.

Tetemeko hilo kubwa la ardhi ambalo limepiga pwani ya Aegean nchini humo na kisiwa cha Samos kilichopo Kaskazini mwa Ugiriki Ijumaa kimesababisha vifo vya takriban watu 27.

Zaidi ya watu 800 wamejeruhiwa kutokana na tetemeko hilo, ambalo liliangusha majengo huko Izmir mji wa tatu kwa ukubwa nchini Uturuki, na kuchochea dhoruba ndogo ya Tsnumani katika Wilaya ya Saferihisar na huko Samos.

Tetemeko ambalo Taasisi ya Kandili imesema lilikuwa katika kiwango cha 6.9 kwa kipimo cha rikta ilipiga jana mchana kwa saa za Uturuki, hasa katika maeneo ya Aegean Kaskazini Mashariki mwa Samos. Tetemeko hilo lilifuatia na mitetemeko kadhaa midogo zaidi ya 400.

Gavana wa Izmir, Yavus Selim Kosger amesema sio chini ya watu 70 waliokolewa kutoka katika kifusi cha jengo lililobomoka na katika majengo mengine 10 yalioanguka.

Wakati tetemeko likitokea wakazi walionekana wakikimbia mitaani katika mkoa wa Izmir wenye wakazi milioni 4, wakiwa wamefazaika.

Aidha, tetemeko hilo lililokuwa na ukubwa wa kipimo cha Richter 7.0, lilisababisha maji mengi kuingia katika Wilaya ya Seferihisar, mkoani Izmir.

Katika nchi jirani ya kisiwa cha Ugiriki cha Samos, mvulana na msichana walikutwa wamefariki katika eneo ambalo ukuta ulianguka.

Rais Recep Tayyip Erdogan amesema kila kinachowezekana kitafanyika ambacho ni muhimu kusaidia juhudi za uokoaji.

*VOA*

# Waziri mkuu abadili uamuzi wa kujiuzulu

**Tripoli, LIBYA**

WAZIRI Mkuu wa Libya, Fayez al-Serraj, amefutilia mbali uamuzi wa kutaka kujiuzulu.

Fayez al-Serraj, alitangaza kufutilia mbali uamuzi wake aliochukuwa hapo awali wa kutaka kujiuzulu Oktoba mwishoni.

Msemaji wa ofisi ya Waziri Mkuu, Galib al-Zaklai, alitoa taarifa kupitia mtandao wa kijamii wa Twitter na kusema kwamba Waziri Mkuu, Serraj amefutilia mbali uamuzi wa kutaka kujiuzulu hadi mazungumzo yanayoendelea kati ya pande mbili husika za Libya yatakapokamilika.

Uamuzi huo wa Serraj ulichukuliwa kufuatia wito kutoka kwa Baraza la Wajumbe wa Tripoli, Baraza Kuu la Serikali, Timu ya Umoja wa Mataifa ya Usaidizi wa Libya (UNSMIL) na baadhi ya nchi rafiki, ambapo alihusiwa aendelee kuhudumu kama Waziri Mkuu wa Libya hadi mazungumzo yatakapokamilika.

Taarifa zaidi zilibainisha kuwa Serraj anatazamia kamati ya mazungumzo itatimiza jukumu lake la kihistoria na kuweka masilahi ya kitaifa mbele, ili kuleta suluhisho katika mgogoro unaoendelea na kuhakikisha amani na upatanishi, bila ya kujali malengo ya kibinafsi.

Mnamo tarehe Septemba16 mwaka huu, Waziri Mkuu, Serraj aliwahi kutangaza kuwa atajiuzulu kutoka kwenye nafasi yake serikalini ifikapo mwezi Oktoba mwishoni.

**TRT**

# Mrithi wa Kansela Ujerumani Januari

**Berlin, UJERUMANI**

KATIBU Mkuu wa Chama tawala cha Christian Democratic (CDU), nchini Ujerumani, Paul Ziemiak, ametangaza kuwa chama hicho kimeamua kufanya mkutano katikati ya mwezi Januari mwaka ujao kumchagua kiongozi mpya.

Baada ya mazungumzo ya kina, wagombea watatu wa nafasi hiyo wameitaka bodi ya utendaji ya chama hicho kufanya mkutano huo Januari.

Wagombea hao ni mfanyabiashara wa zamani na kiongozi wa CDU bungeni Friedrich Merz, Waziri Mkuu wa Jimbo la North-Rhine Westphalia, Armin Laschet na mtaalamu wa masuala ya mambo ya nje katika chama hicho, Norbert Roettgen.

Mkutano huo wa wanachama 1,001 ulikuwa umepangiwa kufanyika mwezi Desemba 4 ila uliahirishwa Jumatatu kwa sababu idadi ya maambukizi ya virusi vya corona inaongezeka Ujerumani na majimbo ya nchi hiyo yamewekwa vikwazo vipya.

Kuahirishwa kwa mkutano huo kulizua mgawanyiko baina ya wagombea hao watatu huku Friedrich Merz akiwatuhumu baadhi ya watu katika uongozi wa chama hicho kumpinga asiuchukue wadhifa huo.

Lakini Katibu Mkuu Ziemiak ametoa wito wa umoja katika chama.

Chama cha CDU ndicho chama kikubwa zaidi katika Bunge la Ujerumani, Bundestag, na kuwa kiongozi wa chama hicho inaonekana kuwa kama mwanzo wa kuchukua mikoba ya Kansela Angela Merkel kama kiongozi wa serikali ya nchi yenye uchumi mkubwa zaidi Ulaya.

Ujerumani ni sharti ifanye uchaguzi wa shirikisho kufikia Oktoba 24, mwaka 2021.

**DW**

# VAN DIJK

## AIPELEKA LIVER AJAX KWA SCHUURS



**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool inamfuatilia mlinzi wa kati wa Ajax, Perr Schuurs ili kumaliza tatizo lao la beki, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

Liverpool imekuwa kwenye wakati mgumu baada ya kumpoteza mlinzi wao, Virgil van Dijk ambaye aliumia goti na kufanyiwa upasuaji.

Schuurs si jina geni kwa Liverpool kwani nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, alikuwa akiwaniwa kwa muda mrefu na 'Wekundu' hao wa Anfield.

Wakati Van Dijk akionekana atakuwa nje ya dimba kwa kipindi kirefu, Liverpool wanaona kwamba wanatakiwa kusajili beki mwingine ili kuziba pengo hilo.

Awali, Schuurs alikuwa akiwaniwa pale Anfield, lakini hakuna ofa yoyote iliyotumwa kwake.

Hata hivyo, kwa sasa Liverpool imeonyesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili mlinzi huyo.

# ZIDANE

## AFUNIKA KOMBE KWA HAZARD MADRID

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane ni kama amefunika "kombe mwanaharamu apite" baada ya kusisitiza kuwa Eden Hazard hana tatizo licha ya mchezaji huyo kutoshangilia wakati alipoifungia Real Madrid bao.

Hazard alifunga kipindi cha kwanza kwenye mchezo dhidi ya Huesca, likiwa bao lake la kwanza kwa kipindi cha siku 392, wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1, Jumamosi.


Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifunga "bao zuri", lakini hakushangilia na hivyo kuibua maneno kwenye mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, kocha Zidane hakuona kama hilo ni tatizo kwa sababu Hazard ndio kwanza alikuwa anarudi mchezoni kwa mara ya kwanza.

"Nina furaha na mchezo," alisema Zidane. "Alicheza kwa dakika 20 katika mechi iliyopita, lakini leo alicheza zaidi.


"Tunajua ubora alio nao; alifunga bao zuri. Na tulilihitaji zaidi kwa sababu mchezo ulikuwa tofauti sana.

"Yeye kutoshangilia bao hilo si tatizo, kwa sababu jambo la msingi ni kwamba amerudi uwanjani na anaweza kuisaidia timu kushinda."



# CONTE

## ALAUMU INTER KUTOKA SARE



**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amelaumu Inter kwa kushinda kufunga mabao katika nafasi walizozipata wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 na Parma, Jumamosi.

Licha ya kupiga mashuti 25 kwenye lango la wapinzani wao, Inter walilazimika kusubiri hadi dakika ya 92 kupata bao la kusawazisha pale katika dimba la San Siro, kupitia kwa Ivan Perisic.

Raia huyo wa Croatia aliungana na Marcelo Brozovic kwenye orodha ya wafungaji wa Inter ambao walicheza bila Romelu Lukaku na Alexis Sanchez.

Na wakati Conte hakutaka kuwalaumu moja kwa moja wachezaji wake, lakini alisema hakuwa na furaha baada ya kushindwa kufunga katika nafasi walizozipata.

"Si mchezo wa kwanza tuliotawala na kushindwa kufunga. Kama huwezi kufunga kwenye soka, huwezi kushinda," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Bado tulikosa nafasi nyingi za kufunga, tulifanya makosa mengi, na hilo si jambo zuri.

"Tunahitaji kujitathmini kwani nafasi zilikuwa za wazi kabisa na tulitakiwa kuondoka na ushindi mzuri tu."



# RONALDO APONA CORONA

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus imethibitisha kuwa nyota wao, Cristiano Ronaldo, kwa sasa tayari ameshapona baada ya kubainika na virusi vya corona mwezi uliopita na kulazimika kukaa karantini kwa muda wa siku 19.

Ronaldo akiwa karantini alikosa mechi nne ndani ya kikosi chake ikiwa ni pamoja na dhidi ya Barcelona ya mshindani wake, Lionel Messi, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakipoteza kwa kufungwa mabao 2-0.

Staa huyo alibainika kupata maambukizi ya corona akiwa kwenye majukumu ya timu ya Taifa ya Ureno Oktoba 13, mwaka huu.

"Cristiano Ronaldo amefanyiwa vipimo kwa mara nyingine na amebainika kwamba hana virusi vya corona, kwa sasa anarejea kwenye timu hivyo hatajitenga tena kama ilivyokuwa awali," ilieleza taarifa ya klabu hiyo.





## CAF YAAHIRISHA FAINALI YA LIGI YA MABINGWA

**CAIRO, Misri**

SHIRIKISHO la Soka barani Afrika (CAF), limelazimika kuahirisha fainali ya Ligi ya Mabingwa iliyokuwa ichezwe Novemba 6, mwaka huu, kutokana na kucheleweshwa kwa mechi ya marudio ya nusu fainali kati ya Zamalek ya Misri na Raja Casablanca ya Morocco.

Hiyo ni baada ya wachezaji zaidi ya 10 wa klabu ya Raja Casablanca kukutwa na virusi vya corona.

Nusu fainali hiyo ilikuwa imepangwa kuchezwa Oktoba 31, lakini kwa sasa itasubiri hadi wachezaji wa Raja wapone.

Fainali hiyo imesogezwa mbele ili kutoa fursa kwa mechi za kufuzu AFCON zitakozochezwa mwezi huu.

Timu ya Al-Ahly imetangulia kwenye fainali ikisubiri mshindi kati ya Zamalek au Raja Casablanca ambapo katika matokeo ya mechi ya kwanza Zamalek iliongoza kwa bao 1-0 ugenini.



## GRIEZMANN: SARE IMEIKERA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

ANTOINE Griezmann amesema wachezaji wa Barcelona waligadhabishwa baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Deportivo Alaves kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Barca ilishindwa kuondoka na ushindi licha ya kutawala mchezo kwa kipindi kirefu, huku wapinzani wao wakiwa na wachezaji pungufu.

Makosa ya golikipa, Neto yalimwezesha Luis Rioja kuipa uongozi Alaves kabla ya Jota kuonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu kwa kumchezea vibaya Gerard Pique.

Straika wa kimataifa wa Ufaransa, Griezmann alisawazisha bao hilo, lakini 'Blaugrana' hao hawakuweza kupata bao jingine.

"Tuna hasira, hasira kwa sababu tulitaka kupata pointi tatu," alisema Griezmann akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulishindwa kutumia nafasi ya kufunga. Tulikuwa na nafasi nyingi sana, lakini tulifunga mara moja tu.

"Tunatakiwa kuimarika ili kuweza kupata matokeo zaidi. Hii timu inahitaji mabao na kuimarika zaidi."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KUMBADILI MESSI NI NGUMU - SETIEN

Hata viongozi Barca wanamwogopa, kuna wachezaji wanaonekana kama ni nembo ya klabu hivyo...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi ni "ngumu kumdhibiti" pale Camp Nou, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa Barcelona, Quique Setien.

Setien alifukuzwa baada ya Barca kuwa na msimu mbaya wa 2019-20, ambapo klabu iliachia taji la Ligi Kuu kwa wapinzani wao, Real Madrid na kukumbana na kichapo kikali cha mabao 8-2 dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali.

Kocha huyo wa zamani wa Real Betis, Setien nafasi yake ilichukuliwa na Ronald Koeman mwishoni mwa msimu, yeye akiwa amechukua nafasi hiyo kutoka kwa Ernesto Valverde, Januari.

Setien alimsifia Messi, lakini alielezea ugumu alioupata kwa mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or pale Barcelona.

"Nafikiri Messi ni mchezaji bora wa wakati wote," alisema Setien akiiambia El Pais.

"Kumekuwa na wachezaji ambao wako vizuri, lakini yeye ni kijana ambaye amekuwa vizuri zaidi.

"Leo ni ngumu mno kumdhibiti. Mimi ni nani hadi nimbadilishe! Wao wamekubali kwa miaka mingi na hakuna ambaye anaweza kumbadilisha.

"Kuna wachezaji ambao wanaonekana kama ni nembo ya klabu, hivyo ni vigumu mno kumfanya lolote.

"Mifano ipo mingi, angalia wakati wa Michael Jordan, mambo yalikuwa hivyo hivyo katika timu yake ya kikapu kule Marekani.

"Ndivyo ilivyo kwa Messi, huwezi kuamua lolote kwake, kwa sababu hata viongozi wa klabu wanamwogopa."

## KWA UFUPI

**INTER KUMUUZA ERIKSEN**
INTER Milan ipo tayari kumuuza kiungo wake, Christian Eriksen, huku AC Milan, Roma na Lazio zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

**NEYMAR ATAKA KUBAKI PSG**
NYOTA wa Brazil, Neymar, ameiambia Paris St-Germain anataka kubaki klabuni hapo na mazungumzo ya mkataba mpya yameanza kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2022. ***(Foot Mercato)***

**JONES KUTOLEWA KWA MKOPO**
MLINZI Phil Jones mwenye umri wa miaka 28, atatolewa kwa mkopo na Manchester United kwenda Burnley Januari. ***(Daily Star Sunday)***

**ISCO AHUSISHWA EVERTON**
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Isco, mwenye umri wa miaka 28, anahusishwa na kwenda kujiunga na bosi wake wa zamia, Carlo Ancelotti, na mchezaji mwenzake wa zamani, James Rodriguez pale Everton. ***(Sunday Mirror)***

**AHMEDHODZIC AWANIWA CHELSEA**
MLINZI wa Malmo, Anel Ahmedhodzic, mwenye umri wa miaka 21, anawaniwa na Chelsea. ***(Expressen)***

**PIRES AMPELEKA MBAPPE REAL**
KIUNGO wa zamani wa Ufaransa na Arsenal, Robert Pires, anaamini nyota wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, atanufaika kama akienda Real Madrid. ***(Goal)***

**LIVERPOOL YAMFUATILIA SCHUURS**
LIVERPOOL inamfuatilia mlinzi wa Ajax, Perr Schuurs, mwenye umri wa miaka 20, baada ya Mholanzi huyo kuwa na kiwango cha kuvutia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sunday Mirror)***

**GATTUSO KUFUNGWA NAPOLI**
KOCHA Gennaro Gattuso anakaribia kusaini mkataba mpya na Napoli, wakati huu ule wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Italia)***

**ATLETICO KUMSAJILI KONDOGBIA**
KLABU ya Atletico Madrid imekubali kumsajili kiungo wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, Geoffrey Kondogbia mwenye umri wa miaka 27, kutoka Valencia baada ya LaLiga kuwapa ruhusu ya kusajili mrithi wa Thomas Partey, ambaye amejiunga na Arsenal. ***(Cadena Sar, via Metro)***

**ZAPATA ATAKIWA MADRID**
STRAIKA wa Atalanta, Duvan Zapata, anawaniwa na Atletico Madrid, huku kocha, Diego Simeone akitafuta patina wa Luis Suarez. ***(Calciomercato)***

**NDOBELE, MOURINHO WAMALIZANA**
KIUNGO wa Tottenham na Ufaransa, Tanguy Ndombele, mwenye umri wa miaka 23, amesema yeye na kocha Jose Mourinho wameweka pembeni matatizo yao ya msimu uliopita ***(Mail on Sunday)***

**LIVER BADO KWA JOHANNESSON**
LIVERPOOL bado inamfuatilia kiungo wa Iceland, Isak Bergmann Johannesson mwenye umri wa miaka 17, ambaye anaichezea IFK Norrkoping ya nchini Sweden. ***(Expressen)***

**MARTINEZ ATULIZA AKILI INTER**
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 23, hajui nini kitatokea kuhusu mustakabali wake, lakini kwa sasa amesema ana furaha kucheza pale Inter Milan. ***(AS)***

## HABARI MICHEZO

# KOCHA BIASHARA AKIRI YANGA MAJI MAZITO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga kilisababishwa na wachezaji wake wengi kutojiamini, huku baadhi wakicheza nafasi si zao.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Baraza alisema amepoteza mechi hiyo kihalali, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni wachezaji wake kucheza kwa kutojiamini kutokana na kukabiliana na timu kubwa kama Yanga.

"Vile vile kuna baadhi ya wachezaji walicheza kwenye nafasi ambazo si zao na hili kuwapa ugumu kwenye mechi hiyo. Nilifanya hivyo kwa sababu ya kutokuwapo kwa baadhi ya wachezaji," alisema.

Baraza alisema awali alianzisha washambuliaji wawili, Gerald Mdamu na Omary Nassor kwa sababu si vizuri kuanza na mmoja wakati wanachezea uwanja wa nyumbani, lakini baadaye alibadilisha mfumo kutokana na Yanga kuanza kuwaelemea.

"Tulichezesha straika wawili kwa sababu nacheza nyumbani, si vizuri kuzuia wakati uko nyumbani, lakini baadaye Yanga walituelemea, nikaamua kumtoa straika mmoja na kumwingiza Ramadhani Chombo kwa ajili ya kuzuia mashambulizi yao na kutafuta ubunifu zaidi," alisema.

Ni mechi iliyomaliza rekodi nzuri ya Biashara kucheza bila kupoteza kwenye uwanja wake wa nyumbani. Biashara United imeweka rekodi hiyo kwa kushinda mechi nne nyumbani kabla ya mchezo wa tano kukubali kipigo hicho cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga.

Pia ni mara ya kwanza kwa Yanga kushinda kwenye Uwanja wa Karume Musoma tangu Biashara United ilipoanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu wa 2018/19, ikiifunga bao 1-0 msimu wa 2018/19 na sare ya bila kufungana msimu wa 2019/20.

Kwa matokeo hayo, Biashara imeshuka hadi nafasi ya nne kwa pointi 16, ikicheza mechi tisa na kuipisha Simba kwenye nafasi ya tatu ambayo iliifunga Mwadui mabao 5-0 na kupanda nafasi moja juu, ikiwa na pointi 16 pia, lakini ikiwa na mabao mengi zaidi.

**MSITU...**



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya, akidhibitiwa na 'msitu' wa wachezaji wa Mwadui FC, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 5-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam malengo ubingwa hayapoi

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania na kujikuta sasa ikiwa na alama sawa na Yanga kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, Azam FC, imesema bado ipo vizuri katika mbio za kuwania ubingwa msimu huu wa 2020/21 na haitakubali kupoa.

Huku ikiwa mbele kwa mchezo mmoja, Azam ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kutokana na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa ikiwa nayo 11 dhidi ya tisa ya Yanga yenye pointi 22 sawa na vinara hao kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

Tayari Azam imepoteza mechi moja na kutoka sare moja, huku Yanga ambayo imekuwa ikishinda kwa idadi ndogo ya mabao, ikiwa timu pekee haijapoteza mchezo wowote katika ligi hiyo msimu huu.

Kiungo wa timu hiyo, Salum Abubakar 'Sure Boy', kama ilivyo kwa Ofisa Habari wao, Zakaria Thabit 'Zaka Zakazi', amesema ana imani kikosi hicho kitafikia malengo yao ya kutwaa ubingwa huo kutokana na kasi ambayo wameanza nayo na watakayoiendeleza.

"Kila mchezaji anatambua ushindani mkubwa uliopo, bado ninaimani kikosi kinaweza kutimiza malengo ambayo kimejiwekea ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu," alisema Sure Boy.

Lakini Ofisa Habari wa klabu hiyo, Zaka Zakazi, yeye amesema bado wanajambo lao kwa msimu huu na wanaamini litatimia kwa kuwa safari ya ligi bado inaendelea.

"Safari ya ligi inaendelea na sisi tuna kazi ya kufanya, tunaamini kwamba tutafanya vizuri kwa kusaka matokeo ndani ya uwanja kwenye mechi zetu zijazo.

"Tunaomba mashabiki waendelee kutupa sapoti tutafanya vizuri, kila kitu kinawezekana kwa kuwa wachezaji wapo vizuri na benchi la ufundi linaifanya kazi yake vizuri," alisema.

## Namungo yaanza kujipanga kimataifa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thierry, amesema baada ya kupata muunganiko katika kikosi chake, sasa amegeukiwa safu ya ushambuliaji kwa kuiandalia programu maalum ili kuhakikisha inatumia vizuri nafasi za mwisho wanazotengeneza.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Hitimana alisema bado kuna mapungufu katika safu yake ya ushambuliaji, hivyo ameanza kuifanyia kazi mapema kabla ya kuanza kwa ratiba ya michuano ya Kombe la Shirikisho, CAF.

Alisema kutokana na kuwapo kwa muda mfupi wa kupata mechi za kirafiki za kimataifa, anatumia mechi za ligi kuwaandaa washambuliaji wake ili kuhakikisha wanakuwa makini katika nafasi za mwisho.

"Katika mechi zetu tunapata nafasi nyingi za wazi, ila bado umaliziaji ni tatizo hivyo kabla ya kwenda kupata aibu huko mbele, ipo kazi nahitaji kuifanya sasa hivi kuhakikisha wanaimarika," alisema Hitimana.

Alisema kwenye mechi tisa ambazo tayari walishacheza kuna baadhi ya michezo wamekuwa wakipata nafasi nyingi za wazi, lakini walishindwa kuzitumia hali ambayo inampa kazi kubwa ya kuifanya sasa.

"Malengo yetu ni kufanya vizuri katika ligi, licha ya kwamba CAF hawajatoa ratiba ya timu tutazokutana nazo, lakini tayari tumeweka mipango yetu kwenye michuano ya kimataifa ni kupambana na kutopoteza mechi yetu ya kwanza," alisema Kocha huyo.

## Tenisi kurindima Gymkhana Nov. 28

**Na Saada Akida**


CHAMA cha mchezo wa Tenisi Tanzania, kimeandaa mashindano ya siku mbili ya wazi yajulikanayo kama BQ Open, yanayotarajiwa kuanza Novemba 28 hadi 29, mwaka huu, huku yakishirikisha timu za watoto chini ya miaka 18 pamoja watu wenye ulemavu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, mratibu wa mashindano ambaye ni kocha wa timu ya Taifa ya Tenisi kwa wenye Ulemavu, Riziki Salum alisema mikoa mitano, Arusha, Moshi, Morogoro, Simiyu pamoja na wenyeji Dar es Salaam wamethibitisha kushiriki mashindano hayo yatakayofanyika viwanja wa Gymkhana, jijini Dar es Salaam.

"Mashindano haya huwa tunayaandaa Novemba ya kila mwaka, tukiyaalika pia mataifa mawili, Rwanda na Kenya. Mwaka huu kama mambo yataenda vizuri na kama mipaka itafunguliwa (kwa nchi hizo) basi tunatarajia wageni wetu hao kuja kushiriki michuano hiyo," alisema Riziki.

Alisema malengo ya mashindano hayo ni kuchagua wachezaji ambao watàunda timu ya taifa kwa upande wa watoto na wenye ulemavu ambao kwa upande wao wataiwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa inayotarajiwa kufanyia mapema Januari mwakani.

Michezo
Jumatatu Novemba 2, 2020
Nipashe



KUMBADILI MESSI NI NGUMU - SETIEN

HABARI UK 22

KAPOTEA HUYO...




Diogo Jota akiifungia Liverpool bao la usiku 'dakika za mwisho' likiwa ni la ushindi kwenye mechi ya Ligi Kuu England wakati wakichapa West Ham mabao 2-0 katika mchezo huo, uliopigwa Uwanja wa Anfield juzi. **PICHA: MTANDAO**

# MUGALU MIEZI SITA NJE, SVEN ABADILI MFUMO

●●● Awatoa hofu mashabiki akitaja mechi ya Novemba 7 dhidi ya Yanga kuwa...

**Na Saada Akida**

SAFU ya ushambuliaji ya Simba imepata 'balaa' kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Bara inayoendelea, baada ya straika wao, Mkongomani Chris Mugalu sasa kutarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa kipindi cha takriban miezi sita akiuguza majeraha, imeelezwa.

Hali hiyo pamoja na sababu zingine za kiufundi, imemfanya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kuanza kuwazoesha wachezaji wa kikosi hicho kucheza kwa mfumo tofauti wa kutumia viungo pekee katika safu ya ushambuliaji, kwa kumfanya kiungo anayecheza katikati kama 'false nine' namba tisa wa kuibia.

Akizungumza na Nipashe baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Mwadui FC kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Sven alisema kuna habari mbaya kwa Mugalu kutokana na kutarajiwa kuwa nje kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Sven alisema bado hajawa na chaguo la kwanza katika safu yake ya ushambuliaji kutokana na wote kufanya kazi nzuri, ikiwamo Bocco ambaye amerejea akitoka majeruhi na kucheza dakika 60, huku Kagere na Mugalu ambao wote ni majeruhi wakifanya vizuri kila anapowapa nafasi.

"Kwa sasa wengi watahisi nalazimika kumtumia Bocco [John] kwa sababu ya Kagere [Meddie] ni majeruhi ya muda mrefu kidogo, lakini kuna habari mbaya kwa Mugalu, kwa mujibu wa daktari nyota huyo atakaa nje miezi sita akiuguza majeraha aliyonayo," alisema Sven.

Kuhusu kutumia mshambuliaji mmoja, alisema ni kwa sababu viungo wake wanauwezo wa kufunga wanapopata nafasi kama ambavyo walifanya dhidi ya Mwadui FC juzi.

Sven alisema baada ya kuona uwezo wa mchezaji mmoja mmoja ikiwamo viungo wake, imekuwa ikimlazimu kutumia mshambuliaji mmoja kwa sababu kukiwezesha kikosi chake kucheza kwa kushambulia zaidi.

"Ninapotumia washambuliaji wawili na kupunguza viungo, timu inacheza chini, pia washambuliaji hao wanakamiwa, lakini unapotumia mmoja mara kadhaa anapobanwa na mabeki, viungo hutumia nafasi wanazozipata kufunga mabao.

"Kama ilivyo kwa mechi yetu ya leo (juzi), ukimtoa Bocco ambaye ni mshambuliaji aliyefunga mabao mawili, mengine yamefungwa na viungo Ibrahim Ajibu, Said Ndemla na Hassan Dilunga," alisema Sven.

Alisema kutumia washambuliaji wawili kutategemea na mpinzani ambaye anakutana naye, kama atalazimika kubadili mfumo, na kwamba kutokana na uwezo wa viungo wake kufunga, kwenda na mshambuliaji mmoja ndio mfumo wake wa kwanza.

Akizungumzia matokeo ya mechi zilizopita dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting ambazo walifanya vibaya kwa kupoteza pointi sita, Sven alisema kikosi chake sasa kimerejea kuhakikisha wanafanya vizuri wakianzia mchezo dhidi ya Mwadui ambao walicheza vizuri.

"Sasa tunahitaji kurudi katika nafasi yetu, baada ya mechi hii tunaanza mipango ya kujiandaa na mechi zetu mbili zijazo tukihitaji pointi sita, ikiwamo dhidi ya Kagera na baada ya hapo tunahitaji pointi muhimu katika pambano letu la Novemba 7, (dhidi ya Yanga)," alisema kocha huyo ambaye kikosi chake kipo nafasi ya tatu kikiwa pointi sita nyuma ya Azam na Yanga zilizopo kileleni na alama 22.

Simba pia itaanza kuipeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya ratiba ya michuano hiyo kutoka baadaye mwezi huu.

## KAZE NA HESABU KALI KIKOSI YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiendelea kuvuna pointi tatu Kanda ya Ziwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amezidi kupiga hesabu kali za kupanua wigo wa kikosi chake kutokana na ratiba ngumu ya Ligi Kuu Bara kwa sasa, ameeleza.

Tayari Yanga imevuna alama sita ikiwa Kanda ya Ziwa baada ya kuichapa KMC kwa mabao 2-1 katika Uwanja wa CCM Kirumba kabla ya juzi, Jumamosi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine mjini Musoma.

Na wakati Jumatano ikitarajia kushuka katika Uwanja wa Gwambina, Misungwi jijini Mwanza kuwavaa wenyeji wao, Gwambina FC, Kaze amesema wana mechi ngumu zinazowakabili mbele, na hana mchezaji anayeweza kucheza mechi nne mfululizo ndani ndani ya siku 12.

"Nina mechi nyingi na ngumu, lazima wachezaji wapambane na wafanye kazi ngumu ya kusaka ushindi, lakini hakuna anayeweza kucheza mechi zote nne mfululizo ndani ya kikosi kwa wakati huu wa kusaka ushindi.

"Ninachokifanya ni kuona kila mchezaji anacheza na ninawafanyia mabadiliko wachezaji wangu ili kuona kwamba wanaweza kuwa fiti kwa ajili ya mechi zijazo.

**"Kikubwa ninachofurahi ni kwamba kila mmoja anaonyesha uwezo wake ndani ya uwanja na anafanya vile ambavyo ninaelekeza," alisema kocha huyo ambaye tangu atue ameshinda mechi zote tatu alizoiongoza Yanga.**

Yanga ambayo ipo mchezo mmoja nyuma dhidi ya Azam FC iliyopo kileleni kutokana na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa, ina pointi 22 sawa na vinara hao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002